Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 79 No. 205 | RAMAD. - SHAW. 1439 AH | JUNI 2019 | IHSAN 1398 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika wale wanaouza ahadi ya Allah na viapo vyao kwa thamani ndogo, hao ndio hawatakuwa na sehemu katika Akhera, wala Allah Hatasema nao wala hatawatazama siku ya Kiyama, wala Hatawatakasa, nao watapata adhabu iumizayo..
(Aali 'Imraan 3:78)

Ukhalifa Ndio Tumaini Pekee

• Mijadala na Makongamano SI Suluhisho

Siku ya Ukhalifa ni siku muhimu sana katika historia ya Islam kwani baada ya kuvunjika kwa Ukhalifa ulioanza baada ya kifo cha Mtume Muhammadsaw, Kwa mara nyingine tena Ukhalifa ulianza mara baada ya kifo cha Sayidna Ahmadas mnamo 27/05/1908.

Hivyo kila inapofika siku hii ni fursa ya kutafakari na kutoa shukuran zetu kwa Allah kwa kuendelea kuuimarisha Ukhalifa huu ndani ya Jamaat Ahmadiyya.

Wakati tukitafakari fadhila nyingi ambazo Allah Anaendelea kutupa juu ya Ukhalifa basi tujikumbushe kidogo juu ya Ukhalifa.

Allah Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba Atawafanya Makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya Makhalifa wa kabla yao, na



kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri. (24:56)

Aya hii inaeleza ya kuwa Mwenyezi Mungu atainua Makhalifa katika umati huu kama vile alivyoinua makhalifa katika umati wa Musa.

Na pia inaeleza ya kuwa makhalifa hao watafanya kazi ya kuipa nguvu dini, na Waislamuwatakaowakataa watakuwa wavunjao amri.

Na kwa kuwa Nabii Isa alikuwa Khalifa wa Nabii Musa miaka 1300 baada yake, kukamilisha mfano huo, Mwenyezi Mungu amemleta Seyidna Ahmad kuwa Khalifa baada ya Mtumesaw miaka 1300 ili kusimamisha Sheria ya Kiislamu.

Endelea uk. 2

Kwa Nini Baadhi ya Waahmadiyya wa Kuzaliwa ni Dhaifu?

Na **Mwandishi Wetu**

Akiogopeshwa na ripoti nyingi zinazopokelewa kuhusu udhaifu wa baadhi ya watoto wa waasisi na Wanajamaat wenye nyazfa za juu ndani ya Jamaat, Amir (kiongozi) wa Jumuiyya ya Islam Ahmadiyya Nigeria, Dr Mashhud Adenrele Fashola alibainisha mzizi wa sababu ya tatizo hilo.

Dr Fashola ambaye alihutubia kuhusu jambo hili wakati wa hotuba ya Ijumaa katika Msikiti wa Tahir, Ojokoro alitoa maoni kuwa mtazamo wa hali hauhusikani na msingi mbovu uliowekwa na wazazi katika maswala ya kuoa mcha Mungu na mwenza mwenye Imani.

"Kwa hakika ni muda muafaka ya kujichunguza sisi wenyewe kwamba kwa nini mambohaya ya ajabu yanatokea miongoni mwetu. Watoto wa wanajamat hai na wenye mamlaka vilevile hawapatikani ndani ya jamaat. Ni wazi kuwa tumeacha amri za Allah ambazo zinatusisitiza kuwa tuoe wacha Mungu na wenye imani. Kwamba tusioe washirikina wala watu wanaopenda dunia" Amir Sahib alisema.

Mambo mengine yanayopelekea jambo hilo sawa na alivyoeleza Amir sahib ni kuabudu vitu vya kidunia mfano kama Taaluma, kutoshirikiana na wacha Mungu na watu wanyenyekevu wanaojitolea, kushiriki katika uovu, dunia, tabia mbaya na kundi la watu wa kidunia; kutotenda haki na makosa ya wazazi hasa ya kuwapendelea baadhi ya watoto na `kutowajali wengine, kwa kutotambua usawa kwa wote, kustahamili uzembe katika kutoa na kuwatii wanafamilia au kuwazungumza kwa ubaya viongozi wa kiroho na ukosefu wa maarifa ya kweli, tabia njema na ufahamu wa kiroho kuhusiana na Jamaat na Islam kwa ujumla.

Maneno yake ni kuwa, " Sababu nyingine ya watoto kupotea njia ni kuabudu vitu vya kidunia. Baadhi ya wanajamaat wameacha mafundisho ya dini kwa sababu ya masomo ya Kisekula. Pia hawajali kazi za jamaat kwa sababu ya hili. La tatu ni kuwa na ushirikiano na watu wabaya na waovu. Waislam wote wanahitaji kupiga hatua kwa kuwa na watu wema na wacha Mungu. Kutotenda haki na kufanya upendeleo kwa wazazi ni jambo la nne".

Alishauri, "Tukiwa kama Mababa, tunatakiwa kuepuka kutotenda haki, kufanya makosa na upendeleo. Watendee jirani zako na watoto kama wa kwako na dumisha usawa. Usiwadekeze wanao zidi ya watoto wengine."

Sababu ya tano ni kutowafunza watoto nidhamu na mafundisho ya Jamaat. "Yaani kutowaelekeza watoto wahudhurie katika shughuli na matukio ya Jamaat"

Kuondoa tatizo hili ndani ya jamaat, Amir Sahib aliwashauri wanajamaat kuoa tu wacha Mungu na wanajamaat wote(waliooa na wasiooa) wanatakiwa kujikita katika maombi na Istighfar ili kujirekebisha wenyewe kabla kuirekebisha dunia.

Dr Fashola akasema, " Njia moja tu ya kuzalisha watu wenye mabadiliko ni kuoa wanawake wacha Mungu. Jiokoeni wenyewe na familia zenu kutoka katika

Endelea uk. 2

Mfahamu Imam Fakhruddin Razi uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Haiwi Haitakuwa; Simba Kumkimbia Fisi

Juhudi kubwa imefanyika ya kuvitafuta vitabu vifuatavyo bila ya mafanikio yoyote. Maktaba zote za jiji la dar es salaam tumezipekua na hakuna tulichoambulia. Vitabu hivi vilikua maarufu sana katika miaka ya arubaini na umaarufu wake ulitokana na makombora yaliyokuwa wanatupiwa kwa mwanachuoni mahiri wa kiislam Sheikh Mubarak Ahmad.

Kitabu cha kwanza ni cha Sheikh maarufu wa enzi hizo Hajj Hassan Abdul Azizi Al kof kiitwacho Kiswasuil Anbiya. Kama ilivyo ada ya Masheikh wetu hawa hamna hoja yoyote yenye thamani hata ya dafu! Ni matusi na porojo zisizo mikono wala miguu na yote hiyo ni jitihada ya kupinga Nabii wa Mwenyezi Mungu Hadhrat Mirza Ghulam (as). Upuuzi huo wa Sheikh Kof ulipigwa kofi la kitaalam na Sheikh huyo hakudiriki kuinua tena kalamu yake. Ingawaje kitabu chake kilisambazwa sana katika karne hiyo kwahivyo leo kama tulivyoonesha hapo juu hakuna dalili hata kidogo kwamba kitabu hicho kiliwahi kupata pumzi katika eneo hili la Afrika Mashariki. Kimezikwa katika kaburi la sahau kama mwandishi mwenyewe na hii ilikua ni lazima kwani Mwenyezi Mungu ansema kiwafaacho binadamu ndicho kinachodumu.

1942 mzee mmoja kutoka katika visiwa vya Ngazija kwa jina la Sheikh Alli Commorian aliinuka na mkusanyiko wa karatasi aliodhani ni kitabu na kukipa jina la Kalimatul Haq No5. Vijana wa siku hizo walitembea na kitabu hicho wakiranda na kukibeba kama vijana wa leo wanavyobeba simu za mpanguso. Leo hatuna ushahida kama kitabu hicho kiliwahi kuwepo ni Jumuiya ya Ahmadiyya tu iliyo na nakala ya kitabu hicho ikiwa ni kumbukumbiku ni jinsi gani wanaomkataa nabii wa Mwenyezi Mungu wanavyopotea.

Kutoka mji wa kale Mombasa Sheikh Al Amin bin Alli aliinuka na kitabu alichokiita Mirzai jinsi wanawavyodanganya Waislamu watu wenye busara walikipuzilia kwa mbali kitabu hicho kwani mwandishi huyo hata hakufahamu kwamba hao aliowaita Mirzai wanafaamika kwa jina la Ahmadiyya. Lakini pigoi kubwa zaidi mwanae Prof. Alli Al Amin Mazrui kinyume na baba yake alisifu sana kazi inayofanywa na Ahmadiyya na akasifu sana tafsiri ya Qur an tukufu Iliyotolea na Sheikh Mubarak Ahmad.

Wakati Masheikh tuliowataja hapo juu na vitabu vyao wamezikwa katika kaburi la sahau kazi zote za Sheikh Mubarak Ahmadi zinazidi kung'ara na kupata umaarufu. Vitabu vyote alivyoviandika na vingine kuvitafsiri kwa lugha ya kiswahili kwa hivi sasa ni lulu zenye thamani. Tayari kuna kitabu juu ya maisha yake na anakumbukwa kwa mapenzi makubwa pamoja heshima. Hivi karibuni kimetoka kitabu Historia Ya Ahmadiyya Tanzania ambacho kinaeleza mchango mkubwa wa mwanachuoni huyo katika maendeleo ya kiroho na kimwili kwa wananchi wa Afrika Mashariki. Sheikh Mubarak Ahmad anakumbukwa kwa mapenzi na heshima kubwa wakati wapinzani wa manabii wa Mwenyezi Mungu hakuna anayewakumbuka kwani siku zote wanamwisho mbaya

Kwa Nini Baadhi ya Waahmadiyya wa Kuzaliwa ni Dhaifu?

Kutoka uk. 1

Jahanamu. Hili linaweza kufikiwa kwa kuwa mfano wa kufanya mema na kuwa mwenye huruma, kudumu katika ibada na kuchika maonyo.

Unatakiwa uwe mvumilivu na msamehevu. Warekebisheni wake zenu na wale muwapendao ambao wanatamani vitu vya kidunia. Shirikianeni wa watu wema na juu ya yote waombeeni wake zenu na watoto."

Amir sahib, pia alionya kuwa utatuzi wa tatizo hili hauishii kwa wazazi walioathiriki pekee. Bali kwa haki ni jukumu letu sote kwa pamoja na baadhi ya mambo kuyazuia mapema,wote mnashauriwa kuwa msiwaachie majukumu wazazi walioathirika wenyewe tu. Ni jukumu letu kuwaangalia wajane na watoto yatima wa wanajamaat. Wakienda kinyume, tutawajibika katika hilo. Amir, Maraisi na viongozi wa tanzim wanatakiwa kuhakikisha wanaziokoa familia za marehemu waliokuwa Mashuhuri na wanajamaat hai. Malipo ya jambo hili ni makubwa mno.

" kwa hakika ni upumbavu kufikiri kuwa watoto wa marehemu sio wa kwetu. Hivyo, kila mtoto wa Kiahmadiyya ni mtoto wetu. Kwa sababu tunaamini kuwa binaadamu ni wa moja, itakuwa ni kosa la jumla ikiwa watoto wa marehemu hawapatikani ndani ya Jamaat."

Akitoa ushauri kwa kunukuu marejeo kutoka katika kitabu cha Masih Aliyeahidiwa(a.s) " Utakaso wa Roho", Dr Fashola alinukuu, " haitegemeinikwakiwango gani ni tajiri, kwa kiwango gani unaufahamu, kwa kiwango gani cha taalumu yako au kama mtaalamu wa dini, na sio ni kwanamna gani nzuri unavyosoma Qurani tukufu. Na sio ni kwa nafasi gani uliokuwa nayo ndani ya jamaat au kujitolea kwako kama Mbashiri, Mwalimu au Daktari. Lakini sawa na Masih Aliyeahidiwa(a.s), ndipo ilipofikia kuwa ni kwakiwango gani hulka za kiroho zimeshiakana nawe, kwa kiwango gani umefikia kiwango cha juu cha kujisafisha, na ni kwa kiwango gani unawahurumia viumbe wote, kwa kuanzia na familia yako, jirani zako, wanajamaat na nchi yako.

" Wale ambao wannaojitahidi kufikia viwango vya juu vya kujitakasa watachikama thabiti na Sunna za Mtukufu Mtume(s.a.w) na atakuwa mtiifu na Amri zte za kimbingu. Haswa, watakuwa waangalifu mno na wenye mapenzi juu ya wake zao na watoto na watakuwa waangalizi wao. Wataepukana na chuki, wivu, kutotenda haki kwa usawa na kuvipenda vitu vya kidunia na wataonyesha hali ya uvumilivu, subra, ubinadamu na kujitoa kwa ajili ya Allah tu."

Ukhalifa Ndio Tumaini Pekee

Kutoka uk. 1

Waidha Aya hii inathibitisha ya kuwa Seyidna Abu Bakar[ra] na Seyidna Umar[ra] na Seyidna Uthman[ra] na Seyidna Ali[ra] wote walikuwa Makhalifa wa kweli na walipata msaada kwa Mwenyezi Mungu, na kila mmoja wao alikuwa paa la Uislamu (Mungu awe radhi nao).

Ukhalifa ni taasisi ya juu kabisa katika dini baada ya Unabii, Pia kuna manabii ambao walikuwa Makhalifa, yapo maelezo ya Mtume[saw] kuwa kila alipokufa Nabii ulifuata Ukhalifa.

Leo hii dunia ina kiu ya Ukhalifa, makongamano na mijadala imekuwa ikifanywa juu ya kupata Ukhalifa, lakini Mtume[saw] alisema nini kuhusu Ukhalifa katika Umma wake?

Imesimuliwa na Hudhaifa[ra] ya kwamba Mjumbe wa Allah[saw] alisema:

Unabii utakuwa baina yenu mpaka Apendapo Allah. Kisha atauondoa. Kisha utakuwepo Ukhalifa juu ya misingi ya Unabii hadi Allah Atapopenda uwepo, Kisha atauondoa pia. Kisha utapatikana ufalme wa kuudhi ambao utakuwa mpaka Allah Apendapo uwepo, Kisha Allah atauondoa. Kisha utapatikana ufalme wa mabavu na utaendelea hadi Allah Akipenda uwepo, Kisha atauondoa. Kisha utapatikana Ukhalifa juu ya misingi ya Unabii. Kisha (Mtume[saw]) akanyamaza. (Musnad Ahmad na Mishkaat)

Makongamano na mijadala sio suluhisho la Ukhalifa bali Allah Ataleta Nabii na baada yake Ukhalifa utasimama.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba] ndiye Khalifa wa tano baada ya Nabii Ahmad[as].

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Imam Fakhruddin Razi

banga
wara



Na

Mwl Abdullah

Hamis

Mbanga,

Redio Ahmadiyya,

Mtwara

Abu Abdullah, Abul Fadhl, Muhammad ibn Umar ibnul Husain At Taymiit Tabaristan. Maarufu zaidi kama Imam Fakhrud-din Razi, ni mmoja wa maulamaa wakuu wa Islam wa zama zote, Huyu hutajwa kama; Hujjatul Islam, Shaikhul Islam, Sultanul Mutakallimiin pia Imamul mushakkikiin.

Mwanazuoni huyu mtawa amewatangulia wanazuoni wengi wa zama zake, na hata wa baadaye katika fani mbalimbali. Imam Razi alikuwa bingwa wa fani anuai k.v. Taarikh (Historia), Falsafa, Hisabati, Unajimu, Utabibu, Kalaam (theolojia) na Ufasiri. Kazi yake kubwa kabisa ni Tafsiri ya Kurani Tukufu aliyoiita ***Mafaatihul Ghaib*** ambayo ilikuja kujulikana kama Tafsiirul Kabiir kutokana na upana wa maelezo yake. Hii ni tafsiri kubwa mno ya Kurani Tukufu kupata kuandikwa, na majalada 32. Pia vitabu vyake kama Kitabul Muhassal, Lubabul Ishaarat na Al'ilmul Akhlaq ni kati ya vitabu vyenye umaarufu mkubwa kwa wasomi wa falsfa na sayansi ya Kiislam.

Kutokana na umahiri wake katika nyanja za kielimu, Imam Fakhrud-din Razi alikuwa akizungukwa na kudi kubwa la wanafunzi lililoundwa na watu maarufu kama wafalme, watawala, majaji na masufi.

Imam Fakhrud-din Razi alizaliwa eneo lililojulikana kama Rayy Jibal, anatokana na familia ya kishafi'i yenye mtazamo wa ki ash'ari. Alizaliwa mnamo tarehe 25/Ramadhani/543 Hijiria, sawa na tarehe 26/Januari/1149 Miladiya. Mwalimu wa kwanza wa Imam Razi alikuwa ni baba yake Dhwiyaud din Umar aliyekuwa mhutubu mkuu wa mji wa Ray huko Iran, Imam Razi pia alipewa lakabu ya Ibun Khatwib Ray. Razi alisomeshwa na baba yake hadi pale mzee huyo alipofariki ndipo akaendeleza masomo yake chini ya mwanazuoni mwingine aliyeitwa Al Kamaalul Simnaani kwa muda.

Baadaye alisoma kwa Majid Al Jilli, ambaye baadaye alisafiri na Imam Razi kutoka mji wa Ray hadi Maragha kwa ajili ya masomo ya muda mrefu ya falsafa na 'ilmul Kalam(Theolojia). Inasemwa kuwa Imam Razi aliweza kukisoma kwa ghaibu kitabu kiitwacho Al Shamil fi usuulid din, cha Sheikh Dhiyaud din Al Juwaini, aliyejulikana kama Imamul Haramain aliyefariki mwaka 1085 miladiya. Isinadi ya walimu wake wa Fiq-hi na Usulid din inaungana na Imam Shafi' ibn Idrisa Muhammad, na isinadi ya walimu wake wa Kalam inaungana na Imam Abul Hasan Ash'ari.

Alipohitimu falsafa, theolojia na fani nyingine za Islam, Imam Razi alisafiri hadi Bukhara na Mawaran Nahr (Transoxiana) na kufanya midahalo na machifu wa maeneo hayo ambao walivutiwa sana na kumbukumbu zake, hotuba zenye mvuto na hoja zake zisizopingika, lakini walimtaka atoke katika miji yao.

Imam Razi alilazimika kuishi kwa shida na kificho katika miji hiyo, aliwahi kuugua na kubaki katika hali ya kuhuzunisha kwa muda mrefu kidogo katika madrasa moja isiyojulikana mjini Bukhara. Hata hivyo alikuwa akisaidiwa na mmoja wa marafiki zake ambaye alikuwa akikusanya kiasi fulani cha zaka kutoka kwa wafanya biashara wenzie kwa ajili ya Imam Razi.

Imam Razi aliwahi kuishi Khwarazm kabla ya kurejea mjini Rayy, na huko akaishi na tabibu mmoja mzoefu na tajiri. Tabibu huyu alikuwa na mabinti wawili aliowapenda sana. Baadhi ya riwaya zinasema kwamba Tabibu huyo tajiri aliwaoza mabinti zake hao kwa wana wawili wa Imam Razi, na wakati wa kifo chake aliacha mali zake zote katika mikono ya wana wa Imam Razi. Riwaya hizi inapingana na maelezo ya Ibn Khallikan anayesema kuwa, kutoka Bukhara, Imam Razi alisafiri hadi Khwarazm ambapo alibahatika kukutana na Shah(Chifu) wa huko, Muhammad ibn Takush aliyemfanya Imam Razi kuwa mtu wake wa karibu, alimhusisha katika maamuzi na pia alimpa madaraka ya ngazi za juu. Hivyo Imam Razi alistawi kimaisha katika eneo la Herat, huko akamiliki mali na kupata watoto. Na kwamba wana historia wanakubaliana katika taarifa hii kwamba watoto wa Imam Razi bado walikuwa wanafunzi hata alipofariki. Hii inabatilisha riwaya ile ihusishayo ndoa za wana wa Imam Razi na mabinti wa tabibu.

Imam Razi alipata jina kubwa na kuheshimiwa sana kuokana na uerevu na ufasaha wake wa lugha katika kiarabu na kiajemi. Hata wanazuoni wakubwa kutoka maeneo ya mbali walikuwa wakihudhuria madarasa yake.

Inasimuliwa kwamba siku moja Imam Razi alikuwa akitoa mhadhara katika madrasa yake maarufu mjini Khwarazm, ilikuwa ni siku ya baridi kali, basi njiwa aliyetoroka mikononi mwa ndege mbuai alianguka karibu yake. Imam alimwokota ndege yule na kumpakata, hapo mwanafunzi wake Sharafud din ibn Unain akatunga beti ifuatayo;

Ja-at Sulaimanuz zamaan bishujuuhaa, Wal mauta yamla' min janaahii haafidh.
man nabba-al wurqau, Inna salkum hurmunw wa innaka malja-a lilkha-if.

Njiwa amemjia Suleiman wa zama na malalamiko yake, hali umauti ukiwa umemwangazia kupitia mbawa za upazi wake. Nani aliyemjulisha ndege yule kwamba kwako patakatifu nawe ni kimbilio salama kwa ajili ya mwenye hofu?

ELIMU YAKE

Imam Razi alipiga hatua kubwa katika utafutaji wa elimu ya dini na dunia, aliwaacha mbali mno wasomi wote wa wakati wake. Katika elimu ya falsafa alivutiwa sana na kazi za Muhammad ibn Zakariyya Al Razi, Abu Musa Al Farabi, Abu Ali Ibn Sina na Imam Muhammad Ibn Ahmad Al Ghazali. Ingawa Imam Razi alimheshimu sana Ibn Sina, na hili linaonekeana katika sherehe alizoziandika juu ya vitabu vya ibn Sina, lakini hakusita kutofautiana naye katka mambo mengi.

Imam Razi ametoa huduma kubwa katika umma wa Islam na dunia kwa ujumla kupitia vitabu vyake vilivyotoa mchango wa kutajwa katika fani mbalimbali. Yeye ndiye aliyeipatia umaarufu mkubwa falsafa ya kiislam, aliandika vitabu vyenye elimu ya kina juu ya theolojia, mantiki(logic), usuli, fiq-h pamoja na tafsiri ya Kurani Tukufu. Tafsiri yake ya Kurani iliheshimiwa na kusifiwa hata na wakosoaji wake. Katika Tafsiri hiyo Tafsiirul Kabiir Imam Fakhrud din Razi aliweza kuoanisha mafundisho ya Kurani na dhana mbalimbali za kifalsafa zilizoonekana kupinzana na ufahamu wa waislam wengi katika zama zake.

Weledi wa hali ya juu uliomo katika tafsiri yake ulimfanya mmoja wa wanazuoni maarufu wa fani ya tafsiri, Qadhwi al Qudhwaat, Abul Hassan 'Ali as Subki aseme kuhusu tafsiri hii akiwajibu wakosoaji wa Imam Razi kuwa; Wa ma al amru kadhaa, innamaa fiihi ma'at tafsiiru kullu shai-in. Na jambo haliko hivyo (wasemavyo) hakika katika hiyo kuna kila kitu pamoja na tafsiri.

Umaarufu wa Imam Razi hata hivyo haukuacha kumjengea maadui, aliwahi kuzushiwa tuhuma mbalimbali na wapinzani wake. Miongoni mwa masingizio aliyozushiwa limo hata la mauaji. Kundi moja la lililojiita Al Karraamiyah liliwahi kuzusha uvumi kwamba Imam Fakhrud din Razi alihusika na mauji ya Sultani Shihabud din Al Ghuri, aliyekuwa ni mfadhili wake mkubwa. Sultani huyu aliwahi kumjengea Imam Razi madrasa kubwa huko Hirat ambapo alikuwa akitoa hotuba za ijumaa na mawaidha mbalimbali kwa Sultani na jeshi lake.

Siku moja, Imam Razi alipokuwa akiendelea kutoa mawaidha ndani ya madrasa hiyo, Sultani aliwasili na kuketi karibu na Imam Razi ambaye aliendelea na mawaidha yake hadi aliposema; Ya Sultan! Sultaanuka laa yabqaa wa laa talbiisur razii, wa innaa muraddunaa ilallaah. (Ewe Sultani, usultani wako hautabaki, nawe hautaendelea kuwa pamoja na Razi. Hakika marudio yetu ni kwa Allah) Kauli hii ilimwathiri mno mfalme huyo kiasi kwamba alilia kwa uchungu na kuwafanya wasikilizaji wote wahuzunike na kutiririsha machozi kwa uchungu.

Katika historia yote ya Islam, hakuna mwanachuoni yeyote aliyemsaidia kifedha mfalme yeyote kama Imam Razi alivyomsaidia Sultani Shihabud din Al Ghuri. Idadi kubwa ya madrasa zilijengwa na wafalme wakubwa kwa ajili ya Imam Razi ndani ya himaya ya Shihabud din Al Ghuri, na zilihudhuriwa na idadi kubwa ya viongozi na wasomi maarufu. Kutokana na uwezo wake wa kujenga hoja, aliwafanya watu wengi kuachana na madhehebu yao mbalimbali na kujiunga na madhehebu ya Ahlus Sunna kupitia mahubiri ya Imam Razi. Hivyo akahesabika kuwa ni mujaddid wa Islam katika karne ya sita hijiriyya.

Pia Imam Razi aliwahi kusingiziwa kuwa eti amejifananisha kidaraja na Mtume Mtukufu Muhammad^{saw}. Ilidaiwa kuwa eti aliwahi kusema; *Qala Muhammadut taazii, wa qala Muhammadur razi.* (Amesema Muhammad wa Arabuni, na amesema Muhammad wa Rayy). Shutuma hii ya uongo ilisambazwa na maadui zake, wakijaribu kuwaaminisha watu kuwa Imam Razi amekufuru ili wamtoe katika Islam. Tena malimtuhumu kuwa eti anaharibu mafundisho ya Islam kwa kuzipendelea Falsafa akina Aristotle. Lakini katika kitabu chake alichokiita Kitabun nafs war ruh, Imam Razi amebatilisha tuhuma hizo alipomtaja Mtume^{saw} kuwa Swaahibush shar'iyyah (Bwana wa Imani). Si hivyo tu, bali Imam Razi alidhihirisha heshima yake kwa masahaba na maulamaa waliopita. Pamoja na kiwango cha juu cha uelewa alichokuwa nacho, lakini bado alikaririwa mara kwa mara akisema; Manit tazamma bimadh-habil 'ajaaiz kaana huwal faaiz (Anayeshikilia mwenendo wa wale wa zamani, huyo ndiye mwenye ufaulu.

Wasia wake aliouandikisha muda mfupi kabla ya umauti wake, unabatilisha kabisa shutuma na masingizio ya wapinzani wake. Humo

Endelea uk. 4

Imam Fakhruddin Razi

Kutoka uk. 3

ameweka wazi Imani yake juu ya Islam, utiifu wake kwa Mtume*saw* na heshima yake kwa masahaba ra, alisema; Wa inna diiniil islaam wa mutaaba'atu Muhammad wa swahabihi wa aalihi 'alaihi wa 'alaihim salaam, wa inna da-abii huwal qur-aanul 'adhiim, imaamiis sunnatun wa 'alaihimal mu'awal. (Na hakika dini yangu ni Islam na ufuasi wa Muhammad na sahaba zake na aali zake juu yake na juu yao iwe amani. Na hakika dira yangu ndiyo Kurani tukufu na kiongozi chanu ni sunna na juu ya hayo mawili mimi ni mwaminifu).

SAFARI ZAKE

Kwa mujibu wa kitabu chake Risaalatul Munadharah, Imam Razi alikwenda mjini Bukhara mara mbili. Mara ya kwanza ni pale alipokuwa mwanafunzi na kuhama kutoka madrasa moja hadi nyingine katika kutafuta elimu. Lakini ujio wake huu umesahauliwa na waandishi wengi wa historia, hautajwi kabisa. Mara ya pili ni wakati alipokuwa akienda Transoxania kwanza alizuru Bukhara na kufanya mdahalo na Sheikh Nurud din As Saabuuni na Sharafud din Mas'uud ambao walistaajabishwa mno na hoja zake zinazoshawishi na maelezo yake yenye mvuto. Kadhia hii ilitokea mnamo mwaka 582 hijiriyya, sawa na 1186 miladiyya ambapo wanajimu walitabiri kutokea kwa tufani kubwa na kuwafanya watu wengi wachanganyikiwe. Imam Razi alitoa hotuba yenye ufasaha wa hali ya juu kubatilisha utabiri huo na hivyo kuondoa hofu iliyokuwa imewakumba watu wa mji huo. Imam Razi alipita tena Bukhara aliporejea kutoka Samarqand na alijadiliana na Sheikh Radhiud din Nishapuri, amaye alimwelezea kuwa ni mdhaifu katika kuelewa dhana na falsafa za kina, lakini hakuwa na ubishi wala kiburi.

Imam Razi alikuwa mkweli na shujaa katika maongezi yake. Alipofika Ghazna, kwanza kabisa, alihitaji kukutana na mtu aliyeheshimiwa na wenyeji kutokana na elimu na umaarufu. Alifahamishwa kuwa mtu huyo pia anatumia vitabu vya Razi kufundishia. Hapo shauku ya Imam Razi ya kukutana na mtu huyo ikaongezeka, basi akamtumia ujumbe wa kuonana naye. Lakini katika hali isiyo ya kawaida, mtu yule Alimsubirisha Imam Razi kwa muda mrefu, na hata walipokutana hakumwonyesha heshima. Basi ndipo Imam Razi alipoazimia kumpa somo, akamwingiza katika mjadala fulani wa kifalsafa uliomwacha mtu huyo patupu akiwa amehemewa.

Imam Razi aliiheshimu sana elimu kiasi kwamba alipopata nakala ya kitabu cha Sheikh Al Ishraaq kiitwacho Talwihaat alikibusu na kukiweka juu ya macho yake kama mtu avaaye miwani.

'Izzud din Ismail b. Husain Marwazi, Mwanahistoria na mwanafasihi marufu anasimulia kwamba Imam Razi alipotembelea Marw huko Khurasan, alikuwa tayari ni mtu maarufu, na hakuna aliyeweza kufanya mazungumzo naye bila ya miadi (appointment). Anasema; "Nikaomba nafasi ya kuwamo katika sanjari yake na kufanikiwa. Siku moja alinitaka niandike kitabu kuhusu isinadi ya Talibiyyiin (uzao wa Abu Talib), alinisisitiza nikiandike katika lugha nyepesi kueleweka na kukumbukwa ili kwamba naye aweze kunyonya maziwa katika fani hiyo pia. Nilipotaka kumkabidhi kitabu baada ya kukikamilisha, alinilazimisha niketi mahala pake, nililazimika kuketi shingo upande. Alichukua kitabu kile na kuanza kukisoma toka mwanzo hadi mwisho, na kujiridhisha kuwa amekielewa. Basi pia akasema; Wewe ni mwalimu wangu katika tawi hili la elimu nami ni mwanafunzi wako. Na huu ndio utaratibu wa kupokea elimu kwamba mwanafunzi lazima apige magoti mbele ya mwalimu wake. Sasa unaweza kuketi utakapo. Baada ya hapo, nilihudhuria darasa lake kama kawaida naye alitufundisha akiwa kikaoni pake pa kawada.

UPINZANI

Kama ilvyo kawaida, kila mkweli ajaye duniani hukabiliwa na upinzani wa hali ya juu. Na hasa iwapo haiba yake itatishia heshima za wale waliojijengea majina na umaarufu katika jamii. Imam Fakhrud din Razi pia hakuepukana na suna hii. Kundi la Al Karraamiya (Karramites) lilipata mashiko makubwa kwa watu wakati huo. Umaarufu na kukubalika kwa mafundisho ya Imam Razi hakukuwafurahisha wakuu wake.

Maoni ya Imam Razi aghalabu yalipingana na mitazamo ya Mukarramiin hasa kuhusiana na tafsiri ya Kurani Tukufu, Karramiya pia walipinga mno elimu ya falsafa. Kundi hili lilichukizwa na heshima ambayo Sultan Ghiyaathud din aliionyesha kwa Imam Razi. Sultani alimjengea Imam Razi madrasa kubwa karibu na Chuo Kikuu (Jami') cha Herat.

Hapa wakaona kuwa hakuna njia isipokuwa ni kufanya naye mjadala mbele ya Mfalme huyo ili waharibu haiba yake mbele ya Sultani. Inasemwa kwamba Abdul Majid ibn Qudhwah, Kiongozi wa kundi hilo, katika mdahalo huo, alikosolewa mengi na Imam Razi akielezwa kuwa ana uelewa finyu juu ya mafundisho ya dini. Katika mdahalo huo, Imam Razi aliwaathiri sana wafuasi vijana wa kundi hilo kutokana na hoja zake zinazoingia akilini, ufafanuzi wake unaoleweka kirahisi na mantiki zake zinazoshikika kwa wepesi. Bahati mbaya iliyoje! Baadhi ya waandishi walizihesabu hoja za Razi kuwa ni matusi na kashfa dhidi ya mpinzani wake. Eti wanadai kuwa matusi na kashfa hizi ndizo zilizowavutia wafuasi vijana wa muendeleo huo.

Kwa hali ilivyokuwa katika zama hizo ni kwamba viongozi wa kidini walihesabika kama miungu watu, hata kuhoji kauli zao tu ilionekana kama ni utovu wa adabu uliofurutu ada. Yumkini moja ya dhima aliyojipa Imam Razi ni kufutilia mbali desturi hii, hivyo alimkosoa Sheikh Abdul Majid Ibn Qudhwa kwa maneno makali yaliyohesabiwa na baadhi ya watu kuwa ni kashfa au matukano.

Aina hii ya majibu au ukosoaji hutumiwa sana na Manabii na watakatifu wa Allah kwa ajili ya kuwasilisha ujumbe halisi kwa hadhira. Mtume*saw* amewahi kuwataja maulamaa waovu ('ulama-as suu-i) kuwa ni kama nyani na nguruwe.

Baada ya kiongozi wa kundi hilo kushindwa vibaya katika mdahalo huo, waungaji mkono wake walijaribu kulalamika wakidai kuwa kulikuwa na mtusi, kashafa na lugha kali upande wa Imam Razi. Dhwiyaaud din, binamu wa Sultani Ghiyaathud din, aliwatetea wa Karramiya na kulalamikia lugha kali iliyotumika dhidi ya kiongozi wa kundi hilo. Lakini Sultani hakuyapa uzito wowote malalamiko ya binamu yake.

Sakata hili halikuishia hapo. siku iliyofuata, Dhwiyaaud din aliitisha mkutano katika chuo kikuu na alipohutubia mimbarini, alisoma aya ya Kurani Tukufu isemayo; Rabbanaa aamannaa bimaa anzalta wa atba'naar rasuula faktubnaa ma'ash shaahidiin.

Kisha akaanza hotuba yake akisema; "Sisi wafuasi wa Kurani kitabu cha Allah tunafuata na kutii Sunna na amri za Mtume*saw*. Tunatangaza chochote ambacho si kauli ya Mtume*saw* ni upotofu na upuuzi. Bila kumhofu Mungu, kuna kundi la watu linasoma falsafa za Aristotle na mafundisho ya kizushi ya Al Farabi na Ibn Sina, wanawadharau na kuwavunjia heshima watakatifu wa dini." "Jana," aliendelea, "mmeona jinsi gani huyu mtu aitwaye Razi, mwenye uchu wa cheo na madarka, alivyomtusi mzee mcha Mungu mwenye moyo wa nuru. Mzee huyu alitukanwa na kudhalilishwa kwa sababu tu alitetea imani na kusimamia utangazaji wa Hadithi na Sunna za Mtume Mtukufu*saw*." Kisha akalia kwa uchungu na kuamsha hisia za wasikilizaji wake akiwashawishi kuandamana dhidi ya Imam Razi. Sultani alipoona jazba na hamasa ya watu wale, aliamua kuwapoza kwa kuita jeshi na kuwaahidi viongozi hao kuwa Imam Razi atashughulikiwa na mafundisho yake yatapigwa marufuku. Kadhia hii inasemwa kuwa ilitokea mnamo mwaka 595 Hijiriya, sawa na 1198 AD.

Ushindi wa Imam Razi katika mdahalo ule uliwaudhi sana wapinzani wake hata wakakusudia kumuua, alitumiwa barua kadhaa na watu wasiojulikana zimtishia maisha yake. Hivyo Imam Razi aliamua kuondoka Herat na kurejea katika mji wake wa asili Rayy. Zamani aliitwa Ibn Khatib, lakini sasa alihutubia mwenyewe na kufundisha mjini Rayy, akapewa lakabu ya Khaatibur Rayy.

UADUI NA WAISMAILIA

Akiwa mjini Rayy, Imam Razi alikutana na mtihani mwingine kutoka kundi la Shia Imami Ismailia ambao pia walikuwa na nguvu kubwa wakati huo. Hili lilitokana na tabia ya Imam Razi ya kufutu bila woga wala upendeleo kadhia yoyote ya kidini. Kuna wakati aliletewa hoja kuhusiana na baadhi ya mafundisho na itikadi za waismailia, Imam Razi alizivunja hoja zao zote na kama kawaida yake, alitumia lugha kali dhidi yao. Ilionekana kana kwamba anawalaani.

Ndipo Muhammad ibn Hassan, aliyekuwa kiongozi mkuu wa Waismailia huko Almuut, alipomtuma jasusi wake kwenda kumtishia Imam Razi na kumuonya. Jasusi huyu alijifanya kuwa mwanafunzi wa Imam Razi kwa miezi kadha. Siku moja, alipopata nafasi, alimvamia Imam Razi akiwa na kisu mkononi na kumtaka Imam Razi aahidi kwamba hatoyakosoa hadharani mafundisho ya kiismailia na kwamba kwa kufanya hivyo, kila mwaka atapatiwa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kujikimu, la sivyo apewe jeraha la kisu litakalopelekea kifo chake. Imam Razi aliipokea tunu hiyo kwa shingo upande kwa lengo la kuokoa maisha yake tu, na baada ya hapo aliachana na suala la ukosoaji wa itikadi za waismaila hadharani. Ingawa mkuu wa waismalia Abul Fadhwl alikuwa akimpa Imam Razi kile kiasi cha fedha cha kila mwaka kwa niaba ya waismailia, Imam Razi hakujisikia vizuri kupokea posho hiyo. Kila ulipowadua wakati wa kukabidhia kile kitita alijikuta akikosa amani na kujihisi kama mtu asiye huru. Kila mara alilikumbuka lile tukio la kutishiwa kisu, aliihesabu fedha ile kuwa kama rushwa iliyoandamana na vitisho. Kwa hali hii aliamua kuhama katika mji wa Rayy na kwenda kuishi Khurasan.

UHUSIANO NA WAFALME

Tangu mwanzo tulieleza kwamba Imam Fakhrud din Razi alikuwa

Inaendelea uk. 5

Imam Fakhruddin Razi

Kutoka uk. 4

akiheshimiwa hata na watawala kutokana na elimu na ucha Mungu wake. Kwa hivi alikuwa na usuhuba mkubwa na wafalme.

Rafiki yake mkubwa alikuwa ni Sultani Shihabud din Al Ghuri, huyu alikuwa ni rafiki yake wa dhiki na faraja. Kuna wakati alikuwa akimwelelezea rafiki yake huyu kipenzi kuhusiana na mahitaji fulani ya kifedha. Hapo Imam Razi akamkabidhi mfalme huyo mali zote alizokuwa nazo kwa wakati ule. Katika siku za baadaye Imam Razi alikwenda Ghazna kwa mwaliko wa Sultani huyo, ndipo Imam Razi alikabidhiwa kiasi kikubwa cha mali kuliko kile alichokitoa kwa mfalme hapo kabla. Ni kana kwamba mfalme alimkopa na akaamua kumlipa na ziada.

Wakati huo, lile kundi la Karramiya ilikwishapigwa marufuku mjini Herat na Imam Razi akaombwa kuubariki mji huo kwa uwepo wake. Basi hapo Imam Razi akarejea tena Herat, ambapo sasa aliitwa Shaikhul Islam na aliishi hapo akiwa na nguvu, mamlaka na heshima ambayo hakuwahi kuipata shekhe yeyote wa kabla au baada yake. Siku rasmi ya kuwasili kwake mjini Herat, mji mzima ulifanya sikukuu, mkuu wa mji, Husain Kharmiil pamoja na viongozi wengine wa mji huo walimpokea na kumsindikiza hadi katika makazi maalum aliyoandaliwa. Alipelekwa katika kasri lililojulikana kama Aiwan Shaahii ambalo lilitolewa na mmoja wa wanafunzi wake Shah(Mfalme) wa Khwarazmi kama zawadi kwa Imam. Na siku hiyohiyo alitoa mhadhara katika chuo kikuu, akisimama juu ya jukwaa maalum lililoandaliwa kwa ajili yake, hivyo darasa lilionekana kama baraza fulani ya kifalme ambayo mbele yake mkusanyiko mkubwa wa watu ulifanyika. Watumishi wake wa kituruki walisimama katika mistari miwili, viongozi na watu mashuhuri waliketi kulia nakushoto kwake. Sultan Mahmud, mtawala wa Firuzah Koh, binamu wa Sultan Shihabud din Al Ghuri naye alikuwapo na akaruhusiwa kuketi karibu na Imam Razi.

Chuo hicho kilipojaa pomoni, Imam akaanza kutoa mafundisho. Wakati wasikilizaji wake walipokuwa wametekwa akili katika kufuatilia mhadhara wake uliojaa fasaha, ghafla, njiwa alidondokea jukwaani pa Imam akiwa amezidiwa, na ndege mbuai aliyekuwa akimuwinda, alipogumia umati wa watu taratibu aligeuza na kutokomea. Hili ndilo tukio tulilolitaja mwanzo, lililopelekea Ibn 'Unain kutunga lile shairi lake.

SHEKHE WAKE, SHEIKH NAJMUD DIN AL KUBRA

Siku moja wakati ambapo machifu, watawala na maafisa wakuu wa mji walipokuwa wamehudhuria darasa lake, Imam Razi aliuliza iwapo kuna mtu yeyote mashuhuri mjini ambaye hakuweza kuja darasani hapo. Alijibiwa kuwa kuna mtawa mmoja aitwaye Najmud din Al Kubra ndiye aliyebaki bila kuja kumwona Imam Razi. Imam alionyesha mshangao akisema; "Kwa nini hakuja kuniona? Mimi ni kiongozi wa waislam na ni Sheikhul Islam, hata akiwa ni sufi mkuu kiasi gani, alitakiwa kuja kuniona".

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi wa Imam Razi waliandaa dhifa na kuwaalika maulamaa wote wawili, yaani Imam Razi na Sheikh Najmud din. Baada ya kusalimiana Imam alimuuliza Sheikh kulikoni hakuwahi kufika kuonana naye. Sheikh alijibu akisema; "Mimi ni mwanadamu, mhitaji na mpungufu mno wa wema. Hakuna fadhila yoyote ipatikanayo kwa kuonana nami wala shari yoyote ipatikanayo kwa mimi kujiweka nyuma." Fakhru Razi akasema; "Hili ni jibu la kisufi. Sasa kwa kuwa Shari'ah na Tariiqaat vimeunganishwa, basi mwenekano wake halisi lazima udhihirike. Napenda ueleze sababu yenyewe." Najmud din Al Kubra akauliza; "Kwa nini iwe muhimu kuja kukuoana?" Imam Razi akajibu; "Kwa kuwa mimi ni kiongozi wa waislam na ni mwanazuoni." Najmud din akamaka; "Elimu ya kwanza ni kumjua Allah, unamtambuaje Mungu wako?". Razi akajibu; "Kwa dalili mamia." Najm akasema; "Dalili zimeletwa ili kuondoa shaka, je kuna shaka yoyote juu ya uwepo wa Allah, Muumba wa mbingu na ardhi? Allah amewafadhili waja wake kwa nuru isiyo na shaka yoyote iangazayo nyoyo zao, na wanahisi hawahitaji dalili yoyote." Imam Razi aliathirika sana na maelezo haya ya Sheikh Najmud din Al Kubra, hivyo kuashiria kutubu kwake, alishika mikono ya Sheikh Najmud din. Kuanzia siku ile, Imam Razi akaamua kuwa mwanafunzi wa Sheikh yule.

Inaelezwa kwamba Sheikh Najmud din alimtaka Imam Razi kusahau yote aliyoyafahamu, na alikusudia kuvunjilia mbali sanamu la elimu yake. Sheikh huyu alimuathiri Razi kwa nguvu za mwongozo wa ndani wa kiroho. Alipobaini kilichomtokea, Imam Razi alijutia na kulalamikia kutobaini kwake hasara aliyokuwa akiipata, na akamwomba Sheikh wake kumfikisha katika hali aliyo nayo yeye, ingawa Imam Razi hakutaka kuwa darweshi.

Ibn Taimiyah anasimulia kisa alichowahi kuelezwa kwamba, Imam Razi na wafuasi wake, waliwahi kumwambia Sheikh yule kuwa; Yaa Shaikh ballaghnaa annaka ta'allamul yaqiin (Ewe Sheikh imetufikia habari kwamba wewe una elimu ya yakini). Naye akajibu "naam." Imam Razi akauliza; "Unapataje elimu, ilihali mimi nawe tumekuwa tukijadili kwa muda mrefu kubatilisha kile kinachotangulizwa kama hoja?" Yule Sheikh akajibu; "Elimu ni hisia za roho ambazo haina uwezo wa kuzikataa." Wote walipigwa na butwaa na wakayarudia maneno haya ya Sheikh, na mmoja wao akatamani kupata hisia hizo. Sheikh yule alimfundisha mwanafunzi huyo hata naye akapata kuzifikia hisia hizo.

Ibn Taimiyah anaongeza kusema kwamba mwanzoni Imam Razi alikuwa na mtazamo wa kimu'tazila ambapo alipingana na itikadi ya kuamini juu ya sifa za Allah. Sheikh alimfafanulia kwamba ukweli uko pamoja na wale wanaoamini juu ya sifa za Allah. Jambo hili Imam Razi hakuwa akiliamini kabisa katika madhehebu ya Mu'tazila na hakuwahi kulijadili katika hatua yoyote. Ibn Taimiyah amenukuu ushuhuda wa Razi katika maelezo yafuatayo; Wa huwa qadi 'tarafa fii aakhiri 'umrihii, bi-annahu qad ta-ammalat twaraqul kalaamiyyatu wal manaahijil falsafiyyah. Famaa wajadahaa tashfii 'aliilaa walaa tarwii ghaliila, wawajada aqrabat twarqu twariiqatul qur-an. (Naye alitanabahi mwishoni mwa umri wake, kwamba alizingatia njia za hoja na mwenenendo wa kifalsafa. Basi hakuziona zikitibu mgojwa wala kumwonyesha unafuu aliyezidiwa, na akaikuta njia ya karibu zaidi ni njia ya Kur ani.) Ikumbukwe kuwa Ibn Taimiyah alikuwa ni mpinzani wa Imam Razi, hivyo hata alipomrejea, alimrejea kwa lengo la kubatilisha mitazamo ya Razi, labda ni kwa kuwa wahanbali wa zama zake walikuwa na wakati mgumu sana mbele ya hoja za Imam Razi.

Itaendelea toleo Lijalo

Wanachuo Jamia Ahmadiyya Wafanya Ziara ya Mafunzo

Na Sh Abid Mahmood Bhatti
Mkuu Jamia Ahmadiyya.



Wanachuo wa Jamia Ahmadiyya Tanzania wakiwa katika ziara ya mafunzo

Mnamo siku ya Jumanne ya tarehe 30/4/2019 wanachuo wa Jamia Ahmadiyya Tanzania wakiwemo Walimu, Masheikh na wanafunzi walifanya safari ya kimafunzo (picnic) katika moja ya hoteli kubwa na maarufu mkoani Morogoro iitwayo *Highland Hotel* iliyopo nje kidogo ya mji kando kando ya milima ya Uluguru barabara kuu iendayo Mkuyuni.

Kama itakumbukwa safari kama hii zimekuwa zikifanyika kwa kutembelea mbuga ya wanyama mikumi (Mikumi National Park) lakini kutokana na changamoto ya usafiri ilikuwa ikijitokeza mara kwa mara, mwaka huu imeonelewa ni vyema kubadili mwelekeo kidogo.

Siku hiyo safari ilianza majira ya saa nne na nusu ahubuhi na kuwasili saa tano kamili. Miongoni mwa wageni waliojumuika katika safari hiyo ni Amir Jamaat, Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry pamoja na wabashiri wa mikoa mbalimbali nchini.

Wakiwa huko, wanachuo walishiriki katika michezo mbalimbali kama vile mpira wa miguu, kuogelea, kuvuta kamba, mpira wa kikapu. Pia walitembelea sehemu kadhaa za hoteli na kujifunza mengi ikiwemo mashine zinazotumika kufanya kazi na hasa ya kufyeka nyasi.

Kisha sala ya Adhuhuri na Alasiri ziliswaliwa kwa pamoja na mara baada ya sala wanachuo na wageni waalikwa walishiriki katika chakula cha pamoja.

Sambamba na chakula kulikuwa pia na kipindi cha vichekesho (vunja mbavu) ambapo washiriki waliburudika vya kutosha.

Shamrashamra hizo ziliendelea hadi saa 12 kamili jioni ambao ulikuwa ndio muda uliotolewa na uongozi wa hoteli kwa msafara huu.

Mwisho tunamshukuru Amir sahib kwa kushiriki nasi katika ziara hii na tunamuombea Khalifa wetu mtukufu Allah Amjalie afya na siha njema - Amin.

Bustani ya Washairi

MBAYA UTEPETEVU

1. Mpenda maendeleo, kamwe usiwe mvivu
Kila yaumu uchao, tenda kazi si uchovu
Unapojituma cheo, hutokuwa tegemezi
Mbaya utepetevu, huwa nyumba ya kilio

2. Mtangulize Molao, tafuta kwa utulivu
Usitwae vya wenzio, kwa kutumia maguvu
Hasha, kula halalio, usipakae utomvu
Mbaya utepetevu, huwa nyumba ya kilio

3. Huwa nyumba ya kilio, ilosheheni mafuvu
Ndani hamna falio, nani mleta kisamvu
Ni nani mleta gao, papikwe paliwe mbivu?
Mbaya utepetevu, huwa nyumba ya kilio

4. Hautakula walao, wale walao mashavu
Utachapa masalio, masazo ya waangavu
Wale watutumuao, yadi, akili na mbavu
Mbaya utepetevu, huwa nyumba ya kilio

5. Jitahidi uwe nao, wachapakazi shupavu
Wa kadili na wa vyuo, hata wa kutega nyavu
Lima walimavyo wao, lima kwa ukakamavu
Mbaya utepetevu, huwa nyumba ya kilio

6. Uwe wa watafutao, usiwe lepe legevu
Ulegevu kichocheo, cha kufanyiza maovu
Tenda kazi za mafao, kana usiwe mvivu
Mbaya utepetevu, huwa nyumba ya kilio

7. Bora shindana na hao, wanaojifanya ndovu
Walio nyikani mwao, wachakarika wagivu
Nenda sawasawa nao, kwa shughuli lovulovu
Mbaya utepetevu, huwa nyumba ya kilio

Al ustadhi Mhenga Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile, Mbagala Rangi Tatu
Dar es salaam.

VISA VYA DUNIA

1. Kwa jina la Manani, ndilo ninalo anzia,
Sina raha mtimani, jinsi ninavyoumia,
Sijui sababu gani, haya ninayapitia,
Visa hivi vya dunia, kizito sina imani.

2. Tokea hapo zamani, mengi nayavumilia,
Mazuri nayatamani, bado sijaambulia,
Kwa watu sina imani, kwa wanayonifanyia,
Visa hivi vya dunia, kizito sina imani.

3. Na kule pwani kunani, nashindwa kusimulia,
Jinsi walivyonihuni, ndugu wanafamilia,
Kama si somo kitini, mungu alimwangazia, Visa hivi vya dunia, kizito sina imani,

4. Kanzu inahali gani, kama itope kofia?
Tu wapi wa kuwamini, aweze kusaidia, Mcheka nae usoni, kweli kakufurahia?
Visa hivi vya dunia, kizito sina imani.

5. Kheri ya ndege mtini, maisha wafurahia, Na viota vya majani, kwa raha wajilalia,
Ila nyumba ya mwanani, haishi kulingishia,
Visa hivi vya dunia, kizito sina imani.

6. Najiuliza kwa nini, kwa wanacholimbukia,
Na nyumba za duniani, kaburi twajifunzia, Tujue namna gani, kifo kinavyotujia,
Visa hivi vya dunia, kizito sina imani.

7. Waringia kitu gani, kwayo mambo ya dunia,
Jione uko ndotoni, mwili utakukimbia, Nyumba yako kaburuni, we roho utabakia, Visa hivi vya dunia, kizito sina imani.

8. Naujanja wa mjini, kwako haukuanzia,
Wa kwanza mafirauni, mwisho waliujutia,
Na ukiiga za nyani, pia utaangamia,
Visa hivi vya dunia, kizito sina imani.

9. Bora ubaki na dini, Mungu Takuangalia,
Hata uwe masikini, taqwah utajivunia,
Kuendekeza unyuni, chini utadidimia,
Visa hivi vya dunia, kizito sina imani.

10. Nimefika kituoni, hapa ninaishilia,
Sika te watu maini, na matozi wakalia,
Yakidondoka mbinguni, tambua utalipia,
Visa hivi vya dunia, kizito sina imani.

Mwl. Najat Fakim Said Nang'olo
=The Big Boss
Ahmadiyya- Pawaga- Magozi- Iringa

KIJANA

1. Umeikataa shule, unasubiri kurithi
Nyumba zenu ziko tele, unazileta hadithi
Kumbe nawe wale wale, una akili theluthi
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.

2. Unaona Mali nyingi, haushangai kwa nini
Nyumba imara msingi, kujenga twaanza chini
Na hivyo mlivyo wengi, unajiona kwa nini?
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.

3. Akili ilivyo ndogo, wapenda wazazi wafe
Unajiona mdogo, kwa nini wewe usife?
Embu punguza kidogo, hatukuombei ufe
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.

4. Wazazi walipambana, kupata unavyoona
Ubadilike kijana, na uwaombee sana
Usijepata laana, yenye mfano hakuna
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.

5. Una tamba na magari, mizunguko ile ile
Unajiona ngangari, shababi wa kundi lile
Muda ukitahayari, ngoma nayo inogile
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.

6. Mara pombe wanawake, unatuona mabwege
Majigambo kurukuke, umekuwa kivuruge
Kiburi kwako ndo mwake, na macho yako matege
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.

7. Kinachoshangaza sana, wewe mkubwa nyumbani
Wenzako wanakazana, wanapambana shuleni
Akili kuchangamana, wanawaza ukubwani
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.

8. Na hii ni siku zote, kwa wapendao vya dezo
Wanapokuwa popote, wanaanzisha mizozo
Kusengenya kama kote, ndio apate tulizo
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.

9. Badilikeni vijana, nimeshaongea sana
Ongeeni vya maana, pale munapokutana
Kujua sana hakuna, msije kutibuana
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.

10. Beti kumi zinatosha, tuzidi elimishana
Nisije nikawachosha, kisa urari wa vina
Bado nitawakumbusha, kwa mambo yenye maana
Pambana upate vyako, uje utambe vizuri.,

Abdallah S. Kalindima (K-mtoto)
#MMAKONDE MSOMI
kalindimasenior@gmail.com

PEPO NI KAO LA WEMA

1. Tega silcio makini, Shika njia ilonyoka,
Moyo ujaze imani, Upate zidi tukuka,
Tenda wema na hisani, Upate kuimarika
Pepo ni kao Ia wema, Hupenya wenye yakini.

2. Kaahidiwa muumini, Na mola Mwenye shukura,
We tenda merna mumini, pepo ni yako shukura,
Siangukie dunia, Kupenda vyenye kutira,
Pepo ni kao Ia wema, Hupenya wenye yakini.

3. Pepo ni kao la wema, Ndilo tuloahidiwa,
Nasi tusibaki nyuma, Ahadi hitimiziwa,
Maghofira yawe mema, Tukiomba rehemewa,
Pepo ni kao Ia wema, Hupenya wenye yakini.

4. Njia yake ni nyembamba, Juhudi fanywe hima,
Kumuombaye muumba, IIi tupate salama,
Umauti ukitukumba, Atupokee kwa wema,
Pepo ni kao Ia wema, Hupenya wenye yakini,

5. Pepo hii haichaguwi, Tajiriwe masikini,
Vitendo vikisitawi, Mlipaji yu manani,
Yupo mwenye kusitawi, Mmiliki mhisani,
Pepo ni kao Ia wema, Hupenya wenye yakini,

6. Sujuda vema tulia, Tumuombe kwa uchungu,
Ya Rabi Mola jalia, Tufishe kiuchamungu,
Hakika twakulilia, Mmiliki wa dunia,
Pepo ni kao Ia wema, Hupenya wenye yakini,

Madumula Ng'amilo
Iringa

KUIKIMU KAZI HII

Moyo wangu watetema, Mapigo kasi yazidi
Zi kudra za Karima, Twakubali bila budi
Katangulia Namwete, Kaungana na nduguze

Amri,Mosse,Ungando, Mbambwa,Swalehe Nasibu
Makhoha,Makupa, Kondo, Wengine wengi dhahabu
Katangulia Namwete, Kaungana na nduguze

Mmetimiza Waqfu, Mmeacha Mithali
Katu ninyi sio wafu, Kawapokea Jalali
Katangulia Namwete, Kaungana na nduguze

Allah Kawaridhia, Udkhul Jannatii
Nasi twaweka nia, kuikimu kazi hii
Katangulia Namwete, Kaungana na nduguze

Huzuni yangu si kwenu, Je nitaweza kuenzi
Hima, Jasho, chozi zenu, Kweli kubaki simanzi
Katangulia Namwete, Kaungana na nduguze

Shunda Mshundia Wana
Morogoro.

BURIANI NAMWETE

1. Muhammad Ahmad, Sudi wetu Namwete
Kafikiwa na ahadi, Rabi kasema muite
Hivyo Kwake amerudi, Tumwombe tusijute
Buriani Namwete, Bashasha izimikile

2. Mtu mwema wa ibadi, mwenye nguvu si kiwete
Msikivu si mkaidi, wa bashasha kama yote
Safari wasikorudi, kaenda twendako
Buriani Namwete, Bashasha izimikile

3. Mwalimu yako juhudi, tunaifahamu sote
Kamba ya Mola Wadudi, hukuiacha isote
Na shughuli za Mahadi, hukukubali zitote
Buriani Namwete, Bashasha izimikile

4. Mtwara na Bariadi, bali Tanzania kote
Imetushika baridi, nyoyo zimebweta bwete
Qudra hapana budi, imetufika ipite
Buriani Namwete, Bashasha izimikile

5. Bashasha yenye mdadi, ulotupa twokote
Uligawa kama kadi, tuwe ka chanda na pete
Sasa hupo umerudi, tutafanyaje tupate
Buriani Namwete, Bashasha izimikile

6. Tusiache uradi, kumwombea Namwete
Wanawe akina Mudi, an ahli zake zote
Wabakie kwenye kundi, imani si sitesite
Buriani Namwete, bashasha izimikile

7. Mola mwenye Kuidadi, Umhesabie vyote
Ili mizani izidi, na peponi umuweke
Msamha wa kuzidi, Mjalie Namwete
Buriani Namwete, Bashasha izimikile

Na **Musa Awadhi Mpinga**

DAFTARI

Uyalole maajabu, yalo kwenye dafutari
Kila jambo la ghaibu, tunalodhani ni siri
Humo tunayo hesabu, mabaya na ya sururi
Rabi twaomba sahali, iwe hisani yasira

Na **Mahmood Hamsin Mubiru**
Wa Mamba

Mbwa Mwitu Na Kunguru

Palikuwepo na kunguru akiwa amekaa kwenye tawi la mti na kipande cha mkate mtamu uliopakwa samli mdomoni mwake. Mbwa mwitu alimuona kunguru na ule mkate na akaanza kutafakari namna ya kufanya ili aupate ule mkate.

Akasogea karibu na kusimama chini ya mti akitazama juu na akasema, "Ndege msharifu namna gani nimuonaye juu



yangu! Uzuri wake hakuna wa kufanana naye, rangi ya manyoya yake ni tamu sana. Laiti kama utamu wa sauti yake unalingana na uzuri wake, basi bila ya shaka yoyote anapaswa kuwa malkia wa ndege". Kunguru alifurahishwa mno na sifa hizi, na ili tu kumuonyesha mbwa mwitu ya kuwa anaweza kuimba alitoa mlio mkubwa sana. Kipande cha mkate kikamdondoka hadi chini, mbwa mwitu akikiokota kwa madaha sana alisema, "Una sauti dada, naona. Unachohitaji sasa ni akili tu."

. . . . . .

Hadithi hii inatufundisha nini?

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yafuatayo kwa kuyazungushia na Penseli

IHSAN	MWANYA	MKAZO	EIDFUND	ATFAL
IFTAR	ZAGAZA	TARBIYYAT	IJTIMAA	TANZIM
LAILAT	SAMBAZA	AHZAAB	KHUDDAM	ISTIKHARA
FITRI	ENGUA	HAFSA	LAJNA	SASISHA
UHALIFU	TEUA	AMRITSAR	NASRAT	TALAKA

L	K	T	C	R	K	R	N	V	P	N	B	V	G	Q	I	T
Z	K	N	E	P	N	Y	M	K	A	M	M	L	K	X	S	A
D	N	C	I	N	L	A	W	S	C	A	J	K	R	S	T	R
L	M	J	D	G	D	A	H	M	K	C	H	G	T	A	I	B
M	A	N	F	D	T	I	I	A	G	M	L	V	T	M	K	I
H	H	J	U	L	L	Z	L	L	J	Q	D	R	Y	B	H	Y
Q	G	H	N	M	W	A	N	Y	A	H	A	F	S	A	A	Y
Y	K	J	D	A	T	B	F	D	X	T	V	U	V	Z	R	A
S	Y	A	U	B	A	J	I	L	N	L	F	K	M	A	A	T
Z	A	G	M	A	J	J	T	R	W	I	T	A	N	Z	I	M
V	N	S	Z	R	T	W	R	Z	L	T	B	T	E	U	A	Z
E	N	H	I	Q	I	L	I	A	A	I	J	T	I	M	A	A
Q	A	B	L	S	A	T	H	M	Y	G	B	M	N	B	N	X
F	S	C	M	F	H	U	S	M	K	W	A	R	Q	B	R	M
Z	R	W	T	N	L	A	N	A	B	A	W	Z	D	W	L	N
Q	A	A	X	Q	I	F	T	A	R	Q	Z	T	A	R	Q	Z
Q	T	R	P	C	J	R	J	F	D	Z	R	O	G	W	T	C

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Majibu ya Chemsha Bongo la Toleo la Mei: *Hongereni mliopatia yote*

1. D
2. D
3. B
4. B
5. An'aam, Faatiha, Kahf, Saba, Faatir
6. C
7. C
8. B
9. B
10. B
11. C
12. D
13. C
14. C
15. A

Miujiza Katika Mahubiri

Na Mwandishi wetu,

Tumepokea taarifa kutoka kwa Bw. Omari Lisinge wa Tunduru juu ya miujiza iliyotuka katika harakati za mahubiri.

Siku moja miongoni mwa siku za mahubiri, Ansarullah tulijumuika kwa ajili ya kwenda kwenye mahubiri na baada ya kujipanga baadhi ya wahubiri wetu walipita na kugawa vipeperushi vya Jama'at jirani na kituo cha Polisi hapa mjini Tunduru. Katika maeneo hayo, kulikuwa na ndugu waliokuwa wamekaa huku wakiwa na huzuni kwa kijana wao kuwa ameshikiliwa na Polisi pasipo hatia na wakati huo walionesha dalili za kukata tamaa kwani hapakuwepo na dalili ya kijana huyo kutoka katika mikono ya sheria.

Wahubiri wetu waliwaambia ndugu hao kuwa hapa tuna kitabu ambacho kina maombi ambayo kama watayaomba kijana wao anaweza akapona au akaokoka katika matatizo yake. Wahubiri waliwaambia ndugu hao kuwa kwa maombi haya hamuhitaji kwenda kwa mganga au kwenda kwa waganga wa jadi na kufanyiwa maombi au dawa ya kumponya kijana wenu katika matatizo yake.

Kwa kuona kuwa ndugu hao waliwapuuzia wahubiri hao, wahubiri wakaona heri wao wamuombe kijana huyo kwa pamoja wakiwa na hao ndugu. Basi Mwalimu Rajabu Sandali aliongoza maombi na kusoma maombi ya Istihara yaliyoandikwa mwishoni mwa kitabu cha Maombi ya Mtume Muhammad (s.a.w). Kisha wahubiri waliondoka na kuendelea na kazi yao.

Maombi ya wahubiri wetu yalipokelewa kwa kijana huyo kufutiwa mashitaka yote na kuwachiwa huru. Na siku hiyo hiyo muda kidogo baada ya mahubiri ndugu mmoja katika ndugu wale walifika kwa mhubiri wetu mmoja na kumwambia wanaomba kupata kile kitabu cha maombi na kumfahamisha yote yaliyotokea baada ya maombi hayo. Mhubiri huyo alimfahamisha huyo ndugu kuwa hapa saa hizi sina kitabu hicho kwani sisi tulikwisha virudisha sehemu husika. Mwisho ndugu huyo aliambatana na mhubiri wetu mpaka msikitini kwetu na kununua kitabu hicho cha maombi ya Mtume Muhammad (s.a.w).

Wakati mahubiri yalipokuwa yanaendelea, majira ya saa 7:30 mchana, wahubiri wetu walimpatia dereva wa boda boda mmoja kipeperushi cha Jama'at ili akisome. Boda boda huyo akasema nimechoka tangu asubuhi mpaka saa hizi sijapata hata mteja mmoja, wahubiri wetu wakamwabia ukisome kipeperushi hiki kwa makini utapata mteja. Wahubiri waliondoka na kabla hawajafika mbali wakasikia mteja wa boda boda anamwita mwenye boda boda huyo. Na kwa kuwa wahubiri walikuwa hawajafika mbali walirudi na kumwambia mwenye boda boda unaona Baraka za kipeperushi chetu.

Taarifa ya Nazim A'la inazidi kutufahamisha kuwa wakati walipokuwa wanafunga shughuli za mahubiri huko mitaani, iligundulika kuwa kitabu cha Silaha za Mahubiri vilikuwa vimebaki viwili tu na wahubiri wawili wakaamua kuvinunua ili waweze kurejea bila vitabu hivi viwili. Kila mhubiri aliweka kitabu hicho katika mfuko wa shati lake na walitawanyika kwa kila mmoja wao kushika njia yake.

Wahubiri hao waliporejea kituoni kila mmoja anamuuliza mwenzake kitabu cha Silaha za Mahubiri unacho? Wote wawili walijikuta hawanavyo na kila mmoja anatoa hadithi kuwa Bwana nilikutana na mtu akakingania kitabu cha mfukoni mwa shati pamoja na kumfahamisha kuwa hiki ni kitabu changu binafsi lakini bado mteja wa kitabu hicho alikingangania na kukilipia. Nazim A'la akamalizia taarifa yake ya mahubiri kwa kusema kuwa 'Sote tukashangaa kwa jinsi vitabu vya mfukoni vilivyonganganiwa'.

Kuzaliwa Kwa Seyidna Ahmad^{as}



Sheikh Muzaffar Durrani
Rabwah, Pakistan

Baba mzazi wa Seyyidna Ahmad as., Hadhrat Mirza Ghulam Murtadha, alioa kutoka katika ukoo wenye heshima wa Kimughali wa huko Aimma, Wilaya ya Hoshiarpur. Mamake Mtukufu Hudhur aliitwa Charagh Bibi. Yeye alijaa sifa za ukinaifu, ukarimu na kuwasaidia maskini. Alikuwa anatia umuhimu sana kuwalisha maskini na alikuwa akiwatimizia mahitaji ya wahitaji. Hii ilikuwa kawaida yake kwamba maskini yeyote alipofariki, yeye alikuwa anaipeleka sanda nyumbani kwake.

Watoto wa Hadhrat Mirza Ghulam Murtadhaa

Hadhrat Charagh Bibi alimzalia Hadhrat Mirza Ghulam Murtadhaa watoto watano:

1. Murad Bibi: Yeye aliolewa na Mirza Muhammad Beg wa Hoshiarpur. Yeye alikuwa mwenye kupata kashfi na ufunuo.
2. Mirza Ghulam Qadir: Yeye alikuwa kaka wa Seyyidna Ahmad as. Alikuwa na vyeo mbalimbali katika serekali ya Kiingereza. Pia alikuwa Mkurugenzi katika ofisi ya Wilaya yake, yaani Gurdaspur
3. Mvulana mmoja alizaliwa aliyefariki baada muda mfupi.
4. Jannat Bibi: Ndiye aliyezaliwa pacha na Seyyidna Ahmad as, na alifariki haraka.
5. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad Qadiani, Masihi Mau'udi na Mahdi Mtakatifu ambaye sasa takdiri zihusuzo dunia zinaambatana naye.

Kuzaliwa kwa Seyyidna Ahmad^{as}

Alizaliwa katika zama za utawala wa Masingasinga ambapo ilikuwa haihifadhiwi taarifa ya kuweka tarehe ya kuzaliwa, na pia familia yake ilikuwa katika matatizo, kwa hiyo hakuna hati maalum ya tarehe ya kuzaliwa kwake. Hata hivyo, Hadhrat Mirza Bashir Ahmad M.A. alikisia kutokana na baadhi ya maandishi na masimulizi kwamba alizaliwa tarehe 13 Fabruari 1835, sawa na 14 Shawwal 1250 Hijria, siku ya Ijumaa wakati wa sala ya Alfajiri. Jambo hili lafaa kutajwa kwamba pamoja na kuzaliwa kwake zama za ugeni na ukata wa familia yake zikaisha kwa kurudishwa Qadian.



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as}
Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa

Imeshatajwa nyuma kwamba yeye alizaliwa pacha. Binti aliyemtangulia alifariki baada ya siku chache. Kuzaliwa kwake pacha kulikuwa na hekima hii pia kwamba kwa sababu hiyo ilitimia bishara ile iliyoandikwa katika baadhi ya maandiko ya Kiislamu kwamba Mahdi Mau'udi atazaliwa pacha. (Fususul Hikam, cha Hadhrat Muhyiddin ibni Arabi, uk. 36. Tafsiri ya Maulana Al-Fadhil Muhammad Mubarak Ali, chapa ya 1308 Hijria.)

Miaka michache kabla ya kuzaliwa kwake, Mujadidi wa karne ya 13 Hadhrat Seyyid Ahmad Brelawii na Hadhrat Ismaili shahidi walikwisha kuwa mashahidi katika Balakot, Wilaya ya Hazara, na kwa sababu ya utawala wa serikali ya Kiingereza, mafuriko ya Ukristo yalienea kote kote katika India kwa kuacha Panjab. Katika Panjab, kwanza kabisa Wakristo walifungua kituo chao cha mahubiri mjini Ludhiana mnamo mwaka 1835, yaani katika mwaka wa kuzaliwa kwa Seyyidna Ahmad as. Ni ajabu ya kudra ya Mungu kwamba dini ya msalaba ilipoanzisha mfumo wa mahubiri yake katika Panjab, ndipo Mwenyezi Mungu akamfanya mvunja msalaba azaliwe katika Wilaya moja ya karibu ili kuponda kichwa cha fitina iliyokuwa inaibuka. Na alipoamrishwa huyo Mvunja msalaba kupokea Baiati, yeye alichagua mji huo huo wa Ludhiana kwa kuchukua Baiati ya kwanza.

MATUKIO KATIKA PICHA



Watoa mada katika maadhimisho ya mkoa wa Dar es salaamya Siku ya Ukhalifa



Wanajamaat wa Dar es salaam katika maadhimisho ya Siku ya Ukhalifa Masjid Salaam





Kikao kati ya baadhi ya wanajamaat na Amir na Mbashiri Mkuu Masjid Salaam katika mwezi wa Ramadhan



Wanajamaat wa Dar es salaam katika sala ya Idi



Watoto wakipata zawadi za Idi kutoka kwa Amir na Mbashiri Mkuu



Picha ya pamoja ya wanachuo wa Jamia Ahmadiyya Tanzania pamoja na Amir Jamaat walipokuwa katika ziara ya mafunzo.



Wanachuowa Jamia Ahmadiyya Tanzania wakipata staftahi kwa pamoja katika ziara yao ya mafunzo.

Uzinduzi wa Masjid Mubarak

Kutoka uk. 11

kwa kutimiza miradi ya ibada na utakaso wa roho na shabaha ya unyenyekevu". Utakaso wa mwili, adabu za kidhahiri na usawa wa nje, vyote ni muhimu mno. Kisha anasema: "Na ukitafakari utaona ya kwamba falsafa hii ndiyo sawa kabisa kuwa hali za kimwili zinaiathiri roho kwa nguvu sana kama tunavyoshuhudia kwamba ingawaje matendo yetu hutendwa na mwili lakini hayana budi kuziathiri hali za kiroho. Kwa mfano, ikiwa tunaanza kulia hata kama kwa kujikalifisha, mara tutaona machozi halisi yataanza kutiririka machoni na kuathiri moyo ambao utasikia huzuni kwa kuyafuata macho. Kadhalika tukianza kucheka kwa kujikalifisha, mara moyo nao utachangamka (moyo hujaa furaha). Pia imeshuhudiwa kwamba sujuda ya mwili nayo huleta unyenkekevu katika roho pia (wakati mwingine sujuda ya mwili inaleta hali ya unyenyekevu na unyonge). Na kinyume chake twashuhudia pia kwamba tukitembea kwa kukaza shingo na kutokeza kifua, hali hii ya kutembea itazalisha maringo na majivuno. Mifano hiyo inahakikisha kikamilifu kwamba bila shaka yoyote hali za kimwili zinaathiri hali za kiroho".

Halafu chakula nacho huathiri hali ya kiroho kwa hiyo tunatakiwa tule vyakula vya wastani, tusiwe walaji wa nyama tupu wala tusiwe wenye kula mboga peke yake. Imeruhusiwa kula vitu safi vilivyoumbwa na Mwenyezi Mungu lakini hairuhisiwa kupita kiasi bali inatubidi tushike njia ya katikati. Kwa sababu vitu hivi huathiri hali za kikhulka na za kiroho za mwanadamu. Kwa kula chakula safi, khulka za mtu huwa njema na pia mtu huelekea kwenye ibada ya Mwenyezi Mungu. Hadhrat Ahmad[as] alisema: "Ni sifa ya Islam pekee kwamba inatoa mwongozo katika kila jambo. Ni hisani ya Mwenyezi Mungu juu ya watu wote wa dunia kwamba Ameweka kanuni za kulinda afya zetu hadi Anasema "kuleni na kunyweni lakini msipite kiasi katika chakula kwa kuongeza au kupunguza". Kwa sababu hali hii inaharibu uwiano na mwishowe itakuja kuathiri hali za kiroho. Basi mtumishi wa kweli afanyaye ibada kwa kumhalisishia Allah dini, si tu kwamba anajiboresha hali yake ya kiroho na kuimarisha zaidi uhusiano wake na Allah bali anajijenga kimwili pia na kutumia neema za Allah kwa kutafuta radhi Yake. Tena huyo huwa hajali kabisa raha, vyakula na vitu vya dunia bali akinufaika na neema za dunia anajitahidi kupitisha maisha yake ili kupata radhi ya Mola wake. Halikadhalika mwaminio hujitahidi kuwatimizia viumbe wa Allah haki zao. Ni dini tukufu ya kiislam pekee inayofundisha kutoa haki za Mwenyezi Mungu pamoja na haki za viumbe Wake.

Basi jinsi nilivyotangulia kusema kwamba kwa kutoa shukrani kwa Allah kwa kutujaalia makao haya makuu mapya, tunapswa tufanye bidii kunyanyua viwango vya ibada zetu na khulka zetu. Kwa sababu watu wa maeneo haya, majirani zetu na wengine watatutazama kwa mtazamo mpya. Hivyo hatunabudi tuonyeshe mafundisho mazuri ya dini ya kiislamu kwa maneno yetu na matendo yetu. Kama tutapitisha maisha yetu tukizingatia maagizo haya, tutatukwa tunafanya mahubiri makubwa sana na tutapata fadhila na baraka za Mwenyezi Mungu. Hapa yafaa kukumbuka kwamba baadhi ya watu huwa wanawatendea vizuri majirani na marafiki lakini huwa hawatendei vizuri wake zao na watoto wao. Mienendo yao hii sio inayowahusu wao wenyewe tu, naam kwa namna hii inawahusu wenyewe kuwa kutokana na hiyo Mungu Atawakamata lakini mambo haya huwa yanaathiri umoja na utulivu wa Jumuiya. Ukosefu wa utulivu nyumbani huwaathiri watoto ambao badala ya kuwa sehemu nzuri ya Jumuiya katika mustakbali, wanaikimbia Jumuiya na dini. Kwa kueneza ujumbe wa dini ya Mwenyezi Mungu ni muhimu mno kuvilea vizuri vizazi vyetu vijavyo lakini kama tutaonyesha mienendo mibaya, vizazi vyetu vitapotea.

Basi yatupasa tufanye jitihada maalumu kuboresha hali zetu kwa sababu ni mali ya Jumuiya. Watoto huwa wanaona ya kwamba kidhahiri baba yangu ni mtu afuataye dini tena ana sifa nzuri katika Jumuiya lakini akiwa nyumbani mwenendo wake huwa tofauti kabisa. Mtazamo huu unakipoteza kizazi kijacho. Kisha kutokana na ugomvi wa nyumbani, ndugu za mke na ndugu za mume wanazidi kuchukiana na hili ni jambo linaloharibu amani ya jamii. Basi wenye nyumba zilizokumbwa na hali kama hiyo, wajitahidi kurudisha amani na upendo katika nyumba zao bali waamue tutafanya hivyo. Mwenyezi Mungu Ametufanyia hisani kubwa kwa kutuunganisha na Jumuiya, basi tukimtolea Allah shukrani kwa hilo, tujitahidi kuboresha hali zetu na kutenda matendo sawa na mafundisho Yake. Vilevile wanawake wanaohamaki juu ya mambo madogo madogo, wao nao walete mabadiliko mema katika nafsi zao kwa ajili ya malezi ya watoto wao. Muufanye mwezi huu wa Ramadhani kuwa kipambanuzi kwa namna hii ya kwamba mboreshe hali za nyumba zenu kwa baraka za Ramadhani. Bila shaka katika mwezi wa Ramadhani kuna mwamko maalumu kuhusu kufika msikitini kwa ajili ya sala lakini mapambo hasa ya msikiti ni uchamungu kwa hiyo tunatakiwa tujitahidi kuzidi katika uchamungu.

Hadhrat Ahmad[as] aliwahi kusema kuwa tukifuata taqwa, tujitenge na kujionyesha, kiburi na majivuno. Katika kila jambo tujitahidi kutafuta njia za kupata radhi na fadhila za Mwenyezi Mungu na tusiwe miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu Amewachukia na kuzifanya sala zao ziwe sababu ya maangamio yao bali tuhesabiwe miongoni mwa wale wanaopata radhi ya Mwenyezi Mungu na kurithi neema Zake. Shabaha hasa ya Makao haya makuu Aliyotujalia Mwenyezi Mungu ndiyo kuitumikia dini lakini kwa mtazamo wa kidunia pia ni fadhili kubwa sana ya Mwenyezi Mungu. Kama nilivyosema awali tusingeweza kuyapata kwa juhudi zetu binafsi. Kwa sura ya makao makuu haya, Mwenyezi Mungu Ametujaalia neema zote mbili, ya kidini na ya kidunia pia. Basi kwa kuzingatia kila jiha, tunatakiwa tutoe shukrani za dhati kwa Mwenyezi Mungu. Watu wa dunia wanapotazama mradi huu wote, huathirika sana tena wanapofahamu kuwa mradi huu umekamilika kwa fadhili za Mwenyezi Mungu tu hupigwa na butwaa kwa sababu jumuiya yetu ni ndogo na njia zetu za mapato ni chache sana na chochote tunachokifanya tunafanya kwa kujitolea kwa wanajumuiya. Hapo ndipo watu hao wanabaini kwamba hata leo, Yupo Mungu Aliye Hai na Humsaidia Amtakaye. Basi kwa njia hii pia, watu wa dunia nao wanaathirika na mafundisho yetu na kupata mahubiri yetu. Ili kuonyesha dhati ya Mwenyezi Mungu ni muhimu maneno yetu na matendo yetu yalingane na kuwaathiri wengine. Hivyo basi tukitazama mradi huu kwa jiha yoyote ile, tunalazimika kuinama mbele ya Mwenyezi Mungu na kumtolea shukrani zetu kwa kutujaalia kustawisha kijiji hiki kipya. Ingawaje idadi ya watu wa hapa ni sawa na idadi ya watu wa mtaa mmoja au ndogo zaidi lakini kina umuhimu wake wa kipekee kwa sababu ya makao makuu. Mwenyezi Mungu Ametujaalia makao makuu katika eneo hili la dunia ambalo halijui uwepo wa Mungu bali limezama katika ushirikina ili tupange kwa ari mpya mipango ya kusambaza umoja wa Mungu na kukamilisha kazi aliyoianzisha mtumishi wa kweli wa Mtume Mtukufu saw. Kisha ufike wakati ambapo tutaona vijiji na miji ikitangaza umoja wa Mwenyezi Mungu na wale wanaomkashifu Mtume Mtukufu bila hofu, waone fahari juu ya kujumuika chini ya bendera yake na wawe wenye kumsalia. Basi haya ndiyo majukumu yetu sote sio majukumu ya wanajumuiya wa Islamabad peke yao. Kila mwanajumuiya popote pale anapoishi ajitahidi kutafuta mbinu mbalimbali za namna ya kupeperusha bendera ya umoja wa Mungu duniani kote, kuwaleta watu wote chini ya bendera ya Mtume Mtukufu saw, kukamilisha kazi aliyoianzisha Hadhrat Ahmad as na kumsaidia Khalifa wa zama kwa maombi na matendo katika kutekeleza mipango yake mbalimbali.

Mwenyezi Mungu Ametuwezesha kuzindua msikiti huu na makao haya makuu katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Sina taarifa kuhusu zama za makhalifa waliopita lakini katika zama za ukhalifa wangu ni mara ya kwanza kabisa kuwa tunafanya uzinduzi wa msikiti katika mwezi wa Ramadhani. Basi mkijifaidisha ipasavyo na mwezi huu wenye baraka nyingi ambamo maombi hupokelewa, ombeni dua kwa wingi kwa ajili ya maendeleo ya Jumuiya na kutimiza shabaha ya makao haya makuu katika eneo hili la dunia. Makao haya makuu yaendelee kupanuka na Waahmadiya wanaoishi pembezoni mwake wazidi kuongezeka, tushuhudie mandhari ya watu kujiunga na Islam makundi makundi, tuone hila na njama za maadui zikivunjiliwa mbali, njia za kwenda Rabwah zifunguke, njia za kurudi Qadian iliyo nyumba ya Hadhrat Ahmad as zipatikane, pia zifunguke njia za kwenda Makka na Madina maana hiyo ni miji ya bwana wetu na mpendwa wetu Mtume Mtukufu saw na makao makuu ya kudumu ya Islam, pia ujumbe wa Islam ya asili uwafikie na waupokee na kuwa wasadikishaji wa mtumishi wa kweli wa Mtume Mtukufu saw. Mwenyezi Mungu Afumbue macho ya wale wenye chuki bila sababu kutokana na ujinga na Awakamate wale wanaotia chuki na husuda katika mioyo ya watu wa kawaida dhidi ya Hadhrat Ahmad as na Jumuiya yake kwa utukutu au kujitafutia masilahi yao binafsi. Waislamu wakijumuika pamoja kwa mkono wa Hadhrat Ahmad as na kuwa uma mmoja wafuate kwa vitendo mafundisho sahihi ya kiislamu na wasiokuwa waislamu nao pia waje chini ya bendera ya Mtume Mtukufu saw haraka iwezekanavyo.

Uzinduzi wa Masjid Mubarak

Inatoka uk 12

mafundisho yetu na matendo yetu yaende sambamba.

Mwenyezi Mungu Ametupa mafundisho kuhusu misikiti katika Qurani Tukufu. Katika aya nilizozisoma mwanzoni, tumeelekezwa kwenye mambo ya maana sana. Kama tukifuata mambo hayo, tutaitendea haki ibada ya Mwenyezi Mungu na kutimiza haki za viumbe Wake. Katika aya hizi Mwenyezi Mungu Anawaambia Waislamu kwa uwazi kwamba kama mnataka kupata ridhaa ya Mola wenu basi muihalisishe imani yenu, dini yenu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pekee. Ikiwa hamtafanya hivyo, hamtapata maendeleo bali mtatumbukia katika shimo la upotevu. Tutapata kurithi neema za Mwenyezi Mungu kama tutatimiza shabaha ya msikiti na kuhalisisha ibada zetu kwa ajili Yake tu. Tukifutilia mbali mawazo ya kidunia na vipaumbele vyake ndipo baraka za Mwenyezi Mungu zitatuteremkia. Kama tutajitahidi kutekeleza hayo mara tano kwa siku ndipo tutakuwa wenye kuihalisisha dini kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Anatuamuru kutakasa roho zetu na tunaweza kufanya hivyo kwa kumhalisishia dini yetu. Lakini wale wasiojitahidi kujirekebisha na kujisafisha wataanguka katika shimo la upotevu maana hao ni watu waliomfanya shetani kuwa rafiki yao badala ya Mwenyezi Mungu na pia wanadhani matendo yao yako sawasawa na ridhaa ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo hali ya wale wanaomkataa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Maulamaa wabaya wa zama hizi walio wapinzani wetu wametawaliwa na hali hiyo hiyo. Maulamaa hao wanajidanganya pamoja na kuwadanganya watu wengine wa kawaida. Wao wanafikiri kuwa wao ndio wanaoifuata Islam bara bara lakini huwa wanatumia kila hila na njama ili kupta masilahi yao tena serikali nayo huwa inawaogopa. Siku hizi upinzani huu umeshika kasi katika jiji la Karachi nchini Pakistan ambapo hata serikali ikiwaunga mkono maadui, inaendelea kutushinikiza kubomoa minara ya misikiti yetu. Tumejitahidi vya kutosha kuwafahamisha kwamba minara hii ilitengenezwa zamani sana na misikiti hii ilijengwa miaka 50 au 60 kabla ya leo lakini juhudi hizi hazikufua dafu kwa sababu serikali inawaogopa sana maulamaa. Pia wamezidi kuwadhulumu wanajumuiya na kuwaonea na kuwatendea vibaya. Wamevuka mipaka katika kumkashifu Hadhrat Ahmad^{as}. Na hao ndio watu ambao kuhusiana nao Mwenyezi Mungu Anasema upotevu umehakiki juu yao. Maulamaa wa jina wanaowapotosha watu, bila shaka wanahesabiwa miongoni mwa wale waliotajwa na Mtume Mtukufu saw kuwa katika zama za mwisho misikiti itajaa watu kidhahiri jinsi tuonavyo misikiti ya wengine lakini itakosa mwongozo na fitina zitatoka kwao na kurejea kwao na wao watakuwa watu wabaya mno chini ya mbingu. Basi katika hali kama hiyo, tuna wajibu mkubwa zaidi kuhalisisha ibada zetu kwa ajili ya Mungu na kuionyesha dunia picha nzuri ya mafundisho ya dini tukufu ya kiislamu. Mwenyezi Mungu Hutufungulia milango mipya ya kueneza uzuri wa mafundisho ya asili ya kiislamu na makao yetu haya makuu ni pete moja ya mnyororo huu. Kwa hiyo yatupasa tuelewe na kuzingatia majukumu yetu. Kama ingekuwa juhudi ya mtu binafsi au ya Jumuiya, makao haya makuu yasingeweza kupatikana bali ni fadhili za Mwenyezi Mungu pekee zilizotujaalia makao haya makuu mapya.

Katika mwezi wa Ramadhani, wakati Mwenyezi Mungu Ametutengenezea mazingira mazuri ya kunyanyua viwango vyetu vya kiroho, tunapswa tufanye jitihada za dhati kuhalisisha dini yetu kwa ajili Yake.

Safari moja Hadhrat Ahmad^{as} akieleza namna ya kumhalisishia Allah dini alisema "Imetajwa katika Qurani Tukufu ๏๏๏๏๏ ๏๏๏๏๏๏ ๏๏ ๏๏๏๏๏ mumkumbuke Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi na mtafakari juu ya hisani Zake. Inatakiwa iwepo ikhlasi, hisani na mwelekeo wa namna hii kuwa Yeye ndiye Mola wa pekee na Mweza wa yote. Hakika muhtasari wa kanuni ya ibada ndiyo huu ya kwamba mtu asimame kana kwamba anamwona Mwenyezi Mungu au Mwenyezi Mungu Anamwona, ajitenge na kila uchafu na ushirikina na azingatie adhama Yake na ulezi Wake". Kisha Hadhrat Ahmad^{as} anasema: "Amwombe Allah kwa maombi ya Mtume Mtukufu saw na maombi mengine na afanye sana toba na kuomba ghofira na akiri mara kwa mara udhaifu wake ili apate nafsi iliyotakasika na ajenge uhuisano wa kweli na Allah na kujipoteza ndani ya mapenzi Yake".

Basi mtakapoihalisisha dini na ibada kwa ajili ya Mungu ndipo mtajaaliwa nafsi iliyotakaswa na mtapata nafasi ya kurekebisha hali zenu na mtaitendea haki ibada ya Mwenyezi Mungu na mtajitahidi kufuata mafundisho ya Mwenyezi Mungu kwa kutimiza haki za viumbe Wake.

Ndugu fulani alinionyesha video moja kutoka kwenye mtandao wa kijamii ambayo inawaonyesha Waislamu wakijumuika na kujipanga kwa ajili ya futari kisha kwa sababu fulani au huenda kwa sababu ya chakula, mara wakaanza kutukanana halafu kugombana na kupigana wao kwa wao. Wanavutana na kuchaniana nguo na kupigana ngumi, vyakula vimetapakaa hapa na pale, hamna heshima kwa wakubwa wala wadogo, wote wanapigana wao kwa wao. Hayo yote wanayafanya wakiwa wamefunga saumu na wakiwa wamevaa kanzu zao kama ilivyo kawaida yao. Ilhali Mwenyezi Mungu Ametuamrisha kuwa mfunga saumu asizungumze yasiyo na maana wala asimrudishie jibu yule anayetaka kupigana naye bali aseme tu nimefunga saumu. Kisha Mwenyezi Mungu Anasema Mimi ndimi malipo ya saumu lakini je Mwenyezi Mungu Atakuwa malipo ya wafunga saumu wa aina hii? Je hao ni watu wanaoipata ridhaa ya Mwenyezi Mungu? Je huo ndio utakaso wa nafsi walioupata kwa saumu? Mambo hayo yanaonyesha wazi kwamba kumwamini Imamu wa zama kuna uzito gani na ilikuwa muhimu namna gani kuwa Imamu wa zama aje kuwaongoza waislamu lakini sasa amewafikia lakini hawataki kumwamini.

Mambo hayo yanatuelekeza kwenye kujichunguza nafsi zetu na kujirekebisha hali zetu. Kama tunakorofishana au tunachukiana juu ya mambo madogo madogo basi tujitahidi kuyaondolea mbali mapungufu haya na tuwe wenye kuitendea haki saumu na tuwe wenye kumwabudu Allah kwa utii kamili na tuwe wenye kufuata maamrisho Yake yote.

Sehemu nyingine Hadhrat Ahmad^{as} alisema: "Hivi leo kitu kinachoitwa Islamu, kimepata hitilafu na kimejaa khulka mbaya (yaani mambo yasiyofaa na ya kipuuzi, khulka mbaya na maovu yamejumuika) lakini ikhlasi ile iliyotajwa katika ๏๏๏๏๏๏ ๏๏ ๏๏๏๏๏ imepaa mbinguni (yaani imefutika duniani). Ukweli, uaminifu, ikhlasi, mapenzi kwa Allah na kumtegemea Yeye zimetoweka duniani. Sasa Mwenyezi Mungu Amedhamiria kuzifufua upya nguvu hizi".

Kisha Hadhrat Ahmad^{as} anasema: "Hizi ni zama ambapo sifa mbaya kama vile kujionyesha, majisifu, majivuno, maringo, kiburi, ufidhuli n.k zimekita mizizi duniani (yaani mabaya haya yote yanaendelea kukithiri) na sifa njema kama vile ๏๏๏๏๏๏ ๏๏ ๏๏๏๏๏ zimepaa mbinguni. Kumtegemea Allah na kujikabidhi Kwake vimepotea duniani (yaani kumtegemea Allah hakupo na kukabidhi mambo kwa Allah jinsi inavyotakiwa afanye mwaminio, hali hii haionekani baina ya waaminio wa jina wa leo ambao wanapigana juu ya mambo madogo madogo. Kwa kifupi sifa njema zimewatoka kabisa); sasa Mwenyezi Mungu Amedhamiria kuzipanda upya mbegu zao".

Kwanza alisema Mwenyezi Mungu Amedhamiria kuzifufua upya nguvu hizi na hapo amesema Mwenyezi Mungu Amedhamiria kuzipanda mbegu zao. Kupanda huku kwa mbegu kumefanywa kwa kumpitia Hadhrat Ahmad^{as}. Mungu Mwenye Enzi Ametekeleza dhamira Yake ya kufufua khulka hizi na kuimarisha ibada na kutoa haki za Mungu na viumbe Wake kwa kumpitia Hadhrat Ahmad^{as}. Sasa sisi ndio tunaotakiwa tuwe majani ya mimea na miti iliyotokana na kupandwa kwa mbegu hizo. Na tunaweza kufanya hivyo kama tutamhalisishia Allah ibada zetu, tutajitahidi kujirekebisha hali zetu baada ya kuona makosa ya wengine na tutamtanguliza Allah juu ya vitu vingine vyote.

Safari moja Hadhrat Ahmad^{as} alisema: "Ikhlasi ni muhimu mno kwa vitendo. Kitendo kisicho na ikhlasi na kisicho na hamu ya kupata ridhaa ya Mungu, hakina thamani yoyote, sala hazina thamani yoyote". Basi hili pia ni onyo kwetu ya kwamba ibada zetu ni kazi bure tu kama hatumhalisishii Allah ibada hizi.

Safari nyingine Hadhrat Ahmad^{as} alisema: "Ieleweke ya kwamba kwa mujibu wa Qurani Tukufu, hali za kimaumbile za mwanadamu zina uhusiano maalumu na hali zake za kikhulka na za kiroho hata namna anavyokula na kunywa huathiri hali zake za kikhulka na kiroho." Kama nilivyopiga mfano wa tukio la futari, hali yao ya kidhahiri huchora picha ya hali yao ya kiroho. Mambo haya yanadhihirisha kwamba hali yao ya kiroho ni mbaya mno na mambo hayo yanatakiwa yawe yenye kutufumbua macho. Hadhrat Ahmad^{as} anasema: "Kama hali hizi za kimaumble zikitumika sawa na maagizo ya sheria, zinageuka kuwa hali za kiroho kama kila kitu kinachoingia katika mgodi wa chumvi kinavyokuwa kama chumvi". Maamrisho ya Mwenyezi Mungu, mambo ya kula na kunywa na khulka za msingi mkizikitekeleza hizo kwa kuzingatia maagizo ya sheria, mtazidi katika khulka njema.

Kisha Hadhrat Ahmad^{as} anaongeza kusema: "Na zinaathiri sana hali za kiroho. Ndiyo maana, Qurani Tukufu, imetia sana maanani utakaso wa mwili, adabu za kidhahiri na usawa wa nje

Endelea uk. 10

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RAMADH. - SHAWW. 1439 AH | JUNI 2019 | IHSAN 1398 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Imesimuliwa na Hadhrat Jabir bin Abdillah^{ra} ya kwamba Mtume^{saw} alisema: Msijifunze elimu kwa nia ya kuona fahari mbele ya wataalamu wengine wala kwa kuringa mbele ya wasio na ujuzi na kuwagombanisha, wala msifanye vikao kwa kuonesha elimu yenu. Atakayefanya hayo atapata moto! Naam moto! (Ubn Majah)

Uzinduzi wa Masjid Mubarak



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akihutubia Ijumaa ya kwanza katika msikiti wa Mubarak katika tukio la ufunguzi wake huko Islamabad, Tilford, Surrey, Uingereza — 17 Mei 2019

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 17/05/2019, baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir ul Mu'minin^{atba} alisoma aya za 30, 31 na 32 za Al A'raaf. Tafsiri ya aya hizi ni kama ifuatavyo:

"Sema, Mola wangu Ameamuru uadilifu na rekebisheni mielekeo yenu ndani ya kila msikiti na mumwombe Yeye kwa utii halisi. Kama Alivyowaumbeni kwanza ndivyo mtarudi. Ameliongoza kundi moja na kundi jingine upotevu umehakiki juu yao, kwa hakika waliwafanya mashetani kuwa marafiki wao badala ya Allah na wanadhani ya kuwa wao wameongoka. Enyi wanadamu shikeni mapambo yenu kwenye kila msikiti na kuleni na kunyweni wala msipite kiasi. Hakika Yeye Hawapendi wapitao kiasi." (7:30,32).

Sifa zote njema zinamthibitikia Mwenyezi Mungu Ambaye leo Anatuwezesha kusali sala ya Ijumaa katika msikiti huu "***Mubarak***" wa Islamabad. Wiki chache zilizopita, nilitangaza ya kwamba Makao Makuu yatahamia huko Islamabad kwa sababu tulianza kupata changamoto katika msikiti wa Al Fazal na utendaji kazi za kiofisi kutokana na nafasi finyu. Kwa hiyo tulihitaji eneo zuri na kubwa kwa ajili ya kuendesha shughuli zetu vizuri na mradi wa Islamabad umetukidhia mahitaji yetu yote kwa kiasi fulani. Baadhi ya watumishi wa Jumuiya na wanaofanya kazi ofisini wamepata makazi yao. Pia nyumba ya Khalifa wa zama imejengwa na ni muhimu mno kujenga msikiti pamoja na nyumba ya Khalifa wa zama ili aweze kufanya shughuli zake za kuongoza sala na kutoa darsa na watu waweze kusali sala nyuma yake kwa urahisi. Leo tunazindua rasmi msikiti huu kwa sala ya Ijumaa ya leo lakini kwa vitendo, baada ya mimi kuhamia hapa Islamabad , msikiti huu ulianza kutumika kwa ajili ya sala na shughuli zingine za kidini. Misafara mikubwa mikubwa ya Khudam, Atfal na Lajna walikuja kutembelea na nikafanya nao vikao mbalimbali katika msikiti huu na vikao vingine vikafanyika katika kumbi zingine ndogo. Ukubwa wa msikiti huu ni mara nne zaidi kuliko msikiti wa Alfazal lakini wakati wa misafara ya watu tulimaizi kuwa hata msikiti huu ni mdogo. Pamoja na msikiti huu pana ukumbi mmoja mkubwa uelekeao kibla ambapo watu walikuwa wanasali sala. Kwa vyovyote vile, madhumuni hasa ya kueleza hayo yote ni kwamba kwa fadhili za Mwenyezi Mungu, Jumuiya ya Waislamu Waahmadiya inaendelea kujenga misikiti katika Uingereza na katika nchi mbalimbali duniani. Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu, katika miaka 10 au 15 iliyopita, Jumuiya ya Waislamu Waahmadiya duniani imepata mwamko mahsusi katika kujenga misikiti lakini msikiti huu ambao nimeupa jina la "***Mubarak***", una umuhimu wake wa kipekee kwa sababu pana makazi ya Khalifa wa zama, makazi ya watumishi 29 au 30 wa Jumuiya kwa sura ya nyumba nzuri na ofisi ninazowasiliana nazo kila siku. Kwa kifupi, eneo hili na msikiti huu ni makao yetu makuu na una umuhimu wake.

Mwenyezi Mungu Aufanye msikiti huu uwe kivuli cha msikiti wa "***Mubarak***" na uwe wenye kuvuta fadhili za Allah na uwe Mubarak (uliobarikiwa) kwa kila namna. Tulipokuwa tunashauriana kuhusu jina la msikiti huu, majina mengine kadhaa yalipendekezwa lakini siku moja ufunuo huu wa Hadhrat Ahmad^{as} ukaja mbele yangu ghafla na ukawa chanzo cha kutoa jina la msikiti huu nao tafsiri aliitoa Hadhrat Ahmad^{as} mwenyewe ndiyo hii: "***Umebarikiwa na umebarikiwa msikiti huu na kila kazi, itakayofanyika humo itakuwa na baraka***". Mwenyezi Mungu Ajaalie kuwa maombi aliyoomba Hadhrat Ahmad^{as} katika msikiti Mubarak wa Qadiani, matakwa yake na hamu yake ya kusambaza mafundisho ya kiislamu duniani kote na kupata ushindi, yaendelee kuufikia msikiti huu pia. Makao makuu haya na msikiti huu, daima uendelee kueneza umoja wa Mungu na mafundisho ya Islam katika Uingereza, Ulaya na nchi zote za dunia. Kuhamia kwa makao makuu hapa kuwe na kheri kwa kila namna na mipango yote ya Khalifa wa zama iendelee kupata baraka na fadhila za Mwenyezi Mungu na pia baraka zilizohusika na msikiti Mubarak wa Hadhrat Ahmad^{as} ziendelee kuushukia msikiti huu.

Hadi jana nilikuwa sijui ya kwamba wakati wa ujenzi wa msikiti wa Mubarak huko Rabwah, Hadhrat Musleh Mau'ud ra alisema haya kuwa msikiti huu utakuwa kivuli cha msikiti Mubarak wa Qadiani. Kwa muda mrefu, Ukhalifa ulikaa huko Rabwah na hata leo zipo ofisi za kimakao makuu lakini tangu miaka 35 iliyopita, ukhalifa ulihamia hapa Uingereza na kulikuwa na haja ya ofisi mpya, vitu vya kisasa, majengo mapya na msikiti mpya. Kutokana na sheria ya nchi ya Pakistan, Ukhalifa ulilazimika kuhama na kuhamia Uingereza ambapo kwa kutimiza mahitaji ya Jumuiya, Mwenyezi Mungu Alitufungulia milango mipya ya maendeleo na mafanikio. Mwenyezi Mungu Aendelee kupanua wigo wa neema Zake Alizotushushia. Baraka na fadhila ambazo maadui walidhani watazinyang'anya kwetu, Mwenyezi Mungu Ametujaalia kwa mara dufu zaidi kuliko awali kwa sura ya msikiti huu na makao yetu makuu haya. Hali ya ujinga wa hao maadui wanaojifanya wamiliki na wadhibiti wa bahati ya Ahmadiyya kwa mawazo yao ni kwamba ndugu fulani alinionyesha mwanasiasa wa chama cha PPP akitoa maelezo yake kwenye mtandao wa kijamii kuwa sisi tuliiwekea Ahmadiyya vikwazo na kuizuia isipate kukua lakini serikali hii mpya imewaruhusu Waahmadiya wajenge makao yao makuu katika Islamabad (akimaanisha mji mkuu wa Pakistan ambao pia unaitwa Islamabad). Sasa hiyo ni hali ya akili zao. Kabla ya hapo pia, mwanasiasa wao fulani alitoa maelezo ya kijinga ya namna hii hii kuhusu Jumuiya kisha akaomba radhi akisema nimekosea kutoa maelezo hayo kwa sababu sikuelewa vizuri. Kwa kifupi, hizi ni fikira za watu wa dunia wasiojua kuwa maendeleo ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiya hutokana na fadhili za Mwenyezi Mungu pekee na hakuna serikali yoyote ya dunia iwezayo kuzuia maendeleo yake wala Jumuiya haihitaji msaada wa serikali yoyote kwa ajili ya kupata maendeleo. Sisi tukipata fadhili za Mwenyezi Mungu, tutadumu kushuhudia maendeleo haya maadamu tutafuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu na kujitahidi kutafuta ridhaa Yake.

Hivyo basi yatupasa tujichunguze nafsi zetu siku zote. Wale ambao Mwenyezi Mungu Amewawezesha kukaa katika mji huu mpya au wale wanaojitahidi kupanga mipango ya kuhamia hapa au wanaohamia, wanatakiwa wajitahidi kurekebisha hali zao.... Sasa wakazi wa hapa wameikabili hali mpya na kwa sababu hiyo wao watatutazama kwa mtazamo tofauti. Baada ya Waahmadiya kuhamia hapa, ghafla wakazi wa zamani wamehisi jambo hili na kuanza kueleza waziwazi kuwa nyinyi Waahmadiya mmeelekea kuja kukaa hapa baada ya Khalifa wenu kuhamia hapo. Kwa hiyo mnapaswa mwonyeshe mifano yenu mizuri zaidi kuliko awali na kuwaathiri kwa athari njema. Ikiwa kwa kelele zetu, kutozingatia kwetu sheria za barabarani au sababu nyingine yoyote, majirani zetu wanapata taabu basi tutakuwa tunatoa ujumbe usiopendeza hata kidogo.

Ikiwa hatuhubiri ujumbe wa asili wa Islam kwa vitendo vyetu basi madai yetu ya kumtolea Allah shukrani yatakuwa hayana thamani yoyote. Kumtolea Allah shukrani kunahitaji kwamba

Endelea uk. 11

Miujiza Katika Mahubiri uk. 8